Jumanne Novemba 28, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581508

nipasheTZ nipasheTZ
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com



BARCELONA YAKANUSHA GUNDOGAN KUONDOKA

UKURASA 22

UKURASA WA 3

**Madereva** walia urasimu uhakiki vyeti vyao polisi



UKURASA WA 5

**Mbaroni** tuhuma kuwakata vichwa mama, mwanawe

UKURASA WA 19

**Israel** kuendeleza operesheni kijeshi kuimaliza Gaza





Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa

# Maumivu nauli za mabasi kupanda

• **Daladala**, safari ndefu zapewa siku 14 za pingamizi... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**'USING'OE JINO UNAONGEZA TATIZO'**

MKURUGENZI Msaidizi Huduma za Afya ya Kinywa na Meno kutoka Wizara ya Afya, Dk. Baraka...



MIAKA 36 YA TAMWA

**Waasisi wasimulia walivyoibua Sheria Makosa Kujamiiana**

UKURASA 4





MAKONDA ASEMA

## Gekul ataadhibiwa na CCM kwa kigezo...

UKURASA 2

**MICHEZO** GAMONDI ATAKA NIDHAMU KUIVAA AL AHLY UK.24

**KATUNI** UK.6

# Maumivu nauli za mabasi kupanda

**Na Elizabeth Zaya**

NAULI za mabasi ya mikoani na daladala zitapanda kuanzia Desemba 8, mwaka huu, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetangaza.

Hatua hiyo inatokana na kupanda bei ya mafuta, gharama za uwekezaji na uendeshaji zikijumuisha matengenezo ya magari, kubadilisha matairi, bima, kodi ya mapato, tozo za halmashauri, ada za tozo za LATRA, uchakavu, ukaguzi wa magari na mishahara ya madereva na wasaidizi wao.

Kwa mujibu wa LATRA, nauli hizo zitapandishwa baada ya kufanyika marejeo ya nauli zilizokuwa zinatumika awali na kufanyia kazi maoni yaliyotolewa na wadau wa usafirishaji.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Ahmed Ame, kupitia taarifa yake ya jana, miongoni mwa sababu za kufanya marejeo ya nauli hizo si tu kupanda kwa bei ya mafuta, bali gharama za uwekezaji na uendeshaji zilizotajwa awali.

Sababu zingine ni uwezo wa gari, ujazo, muda wa matumizi ya gari na matairi yake, idadi ya siku za matumizi ya gari kwa mwaka, wastani wa idadi ya safari na idadi ya abiria watakaosafirishwa na kwamba uchambuzi huo ulizingatia uwezekano wa kuendelea kupanda kwa bei ya nishati ya mafuta.

"Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA katika kikao chake cha kawaida cha 12 kilichofanyika Oktoba 25 mwaka huu, ilipokea na kuchambua na kufanyia uamuzi mapendekeo ya menejimenti kuhusu marejeo ya viwango vya nauli za mabasi ya masafa marefu na mijini (daladala).

"Bodi ilijiridhisha kwamba nauli zilizorejewa, zimezingatia mambo ya msingi yatakayofanya huduma iendelee kupatikana na watumiaji huduma waendelee kumudu nauli hizo na kupata huduma ya usafiri," Ame alieleza katika taarifa yake hiyo.

Alibainisha kuwa bodi iliridhika ukokotoaji huo wa nauli ulitumia kiwango cha rejesho la mtaji la asilimia 12 kama baadhi ya watoa huduma walivyoomba ili watoe huduma ya usafiri ulio bora na kwa ufanisi.

Kwa mujibu wa bodi hiyo, baada ya kurejelea viwango vya nauli za daladala, iliamua kwamba kwa umbali usiozidi kilomita 10 ambao awali nauli yake ilikuwa ni Sh. 500, nauli inayopendekezwa ni Sh. 600, wakati kwa kilomita 11 hadi 15 iliyokuwa Sh. 550, inayopendekezwa ni Sh. 700.

Kadhalika, kwa umbali wa kuanzia kilomita 16 hadi 20 ambao awali ilikuwa Sh. 600, kwa sasa inayopendekezwa ni Sh. 800 wakati kuanzia kilomita 21 hadi 25 iliyokuwa inatozwa Sh. 700 sasa inapendekezwa kuwa Sh. 900.

Pia umbali wa kuanzia kilomita 26 hadi 30 ambayo nauli yake awali ilikuwa Sh. 850, inayopendekezwa sasa ni Sh. 1,100 wakati kwa kilomita 31 hadi 35 ambayo ilikuwa Sh. 1,000, inapendekezwa Sh. 1,300. Kilomita 36 hadi 40 ambayo nauli yake ilikuwa Sh. 1,100, sasa wanapendekezwa iwe Sh. 1,400.

Kwa mabasi ya masafa marefu, basi la kawaida kwenye barabara ya lami ambalo nauli yake ilikuwa Sh. 41.29 kwa kilomita, sasa wanapendekezwa iwe Sh. 48.47 kwa kilomita. Kwa basi la aina hiyo kwa barabara ya vumbi ambalo awali nauli yake ilikuwa Sh. 51.61, sasa wanapendekeza kuongezeka ili iwe Sh. 53.32 kwa kilomita.

Basi la kati ambalo nauli yake ilikuwa inatozwa Sh. 56.88 kwa kilomita kwa barabara ya lami, sasa wanapendekezwa iwe Sh. 67.84 kwa kilomita.

Nauli hizo mpya zikipitishwa, zinatarajiwa kuibua maumivu kwa wananchi kwa kuwa kila kunapotokea upandishaji wa nauli, kumekuwa kukishuhudiwa kupanda bei za bidhaa zinazohitaji usafirishaji kutoka eneo la uzalishaji au sokoni kwenda kwa walaji.




Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph (kulia), akitoa maelezo kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (katikati), alipotembelea mradi wa maji Nzuguni jijini Dodoma jana. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Alhaji Jabiri Shekimweri. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kliniki kutibu waraibu dawa za kulevya yafunguliwa gerezani

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, amefungua rasmi kliniki ya Methadone katika Gereza la Kihonda mjini Morogoro.

Kliniki hiyo itahusika na utoaji wa tiba saidizi kwa waraibu wa dawa za kulevya kwa mahabusu na wafungwa magerezani na watu binafsi katika Mkoa wa Morogoro na maeneo mengine ya jirani.

Sambamba na ufunguzi wa kituo hicho kilichojengwa na serikali kwa ufadhili wa mfuko wa dunia (Global Fund) kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Naibu Waziri pia amezindua Jumuiya ya Kimataifa ya Wataalamu Wanaoshughulika na Masuala ya Kinga na Tiba kwa Waraibu wa Dawa za Kulevya nchini (ISSUP).

Akimwakilisha Waziri Jenista Mhagama kuzindua kituo hicho na jumuiya hiyo kwenye Gereza la Kihonda mjini Morogoro, Naibu Waziri Nderiananga alisema serikali itaendelea kutoa elimu na kuzuia uzalishaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya dawa za kulevya na kuendelea kuratibu shughuli za kudhibiti na kupambana na dawa hizo nchini. Aliwataka wananchi kuendelea kukemea kwa nguvu zote matumizi na biashara ya dawa za kulevya na kuahidi serikali kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, vyombo vya ulinzi na usalama, wizara mbalimbali, mahakama na taasisi zingine wataendelea kupambana na tatizo hilo kwa kuwakamata wafanyabiashara wa dawa za kulevya, kutoa elimu sahihi na kuboresha afya za Watanzania kwa kufanya upanuzi wa tiba na huduma za utengamao kwa waraibu nchini.

Naibu Waziri aliwataka wananchi wa Morogoro na maeneo mengine ya jirani kutumia kliniki hiyo kuwapelekea waraibu ili kupata huduma na kusaidia kupunguza madhara yatokanayo na dawa za kulevya miongoni mwa waraibu na jamii kwa ujumla.

"Pia niwaase wazazi na walezi kuwalea watoto katika misingi ya maadili ili kuwaepusha na vitendo viovu ikiwamo matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

"Vilevile, ninazisihi asasi za kiraia pamoja na wasanii kuendelea kutoa elimu kuhusu athari ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya kwa jamii na Taifa bila kuchoka," aliagiza.

Mkuu wa Gereza la Mahabusu Kihonda, Lucas Mboje, ambaye ndiye msimamizi mkuu wa mradi huo, alisema kituo hicho kimegharimu Sh. milioni 506 hadi kukamilika, kikihusisha jengo kuu, uzio, kibanda cha ulinzi, banda la kupumzikia, maegesho, taa zinazotumia nishati ya juu na tangi la maji.

Alisema Jeshi la Magereza linatambua umuhimu wa wafungwa na mahabusu kuwa na afya njema na ndio maana wameruhusu ujenzi huo utakaofaidisha wananchi wa Morogoro na maeneo mengine ya jirani.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini, Aretas Lyimo alimshukuru Kamishna Jenerali wa Magereza Mzee Ramadhani Nyamka kukubali jengo hili lijengwe katika eneo hili la Gereza la Kihonda.

# Makonda asema CCM itamwadhibu Gekul

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeahidi kumchukulia hatua dhidi ya aliyekuwa Naibu Waziri wa Sheria na Katiba, Pauline Gekul, iwapo itathibitika kuhusika na tuhuma za ukatili na udhalilishaji zinazomkabili.

Gekul ambaye ni Mbunge wa Babati Mjini (CCM), anatuhumiwa kutoa maelekezo kwa kundi la vijana kumdhalilisha kwa kumpiga, kumwingizia chupa sehemu ya haja kubwa na kumtishia kumpiga risasi mfanyakazi wake, Hashim Ally.

Novemba 25 mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alitengua uteuzi wa Gekul ingawa taarifa ya Ikulu haikueleza sababu za uamuzi huo.

Jijini Dar es Salaam jana, Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, wakati akijibu swali la waandishi wa habari kuhusu hatua zinazochukuliwa CCM kutokana na kashfa inayomkabili mbunge huyo, alisema:

"Chama chetu kina kanuni, taratibu na sisi ngazi ya taifa tunajua kuna mashina yanayoanza katika ngazi ya tawi alilotokea kwenda mpaka ngazi ya wilaya, mkoa na itakapofika ngazi ya taifa tutatoa taarifa ya kwamba nini kimetokea.

"Kanuni zipo, kuna mamlaka za nidhamu na tuna watu wa maadili. Kama kuna jambo ambalo litabainika, basi taratibu zitafuata mkondo wake, atachukuliwa hatua kwa mujibu wa kanuni zetu za chama."

Makonda pia alisema chama kinawajulisha wajumbe wa kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya CCM kuwa kutakuwa na vikao vya kawaida chini ya Mwenyekiti wake, Rais Samia.

"Kikao hicho kitaanza na semina ya mafunzo kwa wajumbe wa Halmashauri Kuu na kufuatiwa na kikao cha Halmashauri Kuu Novemba 29 mwaka huu. Kitafanyika jijini Dar es Salaam," alisema.

Makonda alisema maandalizi ya mkutano huo yapo vizuri na yamekamilika, hivyo wanachama na wakereketwa wafuatilie kwa kina kikao hicho muhimu kitakachojadili mustakabali wa chama hasa maendeleo ya Watanzania.

"Lengo ni kuwajulisha wanachama ratiba ya vikao ngazi ya taifa. Ni sehemu ya kuongeza chachu kuanzia ngazi ya mashina, matawi, wilaya wanapoona viongozi wao wanakutana kujadili mambo ya mustakabali wa taifa lao katika uhai wa chama, basi na wao wanapata molari ya kuendelea kuishi kwa mujibu wa kanuni kwa kufanya vikao kama ambavyo kanuni zetu zinaelekeza," alisema.

Makonda alisema kikao hicho ni cha kawaida. Kwa mujibu wa ratiba za chama, kunakuwa na vikao vikubwa viwili vya Halmashauri Kuu ambavyo vinakaa kwa mwaka ambacho hufanyika mwanzo wa mwaka na mwisho wa mwaka.

# Biteko: Shirikisheni wananchi uandaaji Dira ya Taifa 2050

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ameagiza Tume ya Mipango kuweka utaratibu wa ushiriki wa makundi mbalimbali ya wananchi na wadau wengine katika kutoa maoni kwenye mchakato unaoendelea wa uandaaji Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

Alitoa maagizo hayo jana alipomwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa katika hafla ya ufunguzi wa Kongamano la Kwanza la Wanamipango 2023 lililofanyika jijini Arusha.

"Tume ya Mipango hakikisheni wananchi wote washiriki kikamilifu kutoa maoni yao kuhusu Tanzania wanayoitaka katika miaka 25 ijayo.

"Maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050 yameanza na kutokana na umuhimu wa Dira kwa Taifa letu, wanamipango na wadau wote ni muhimu kila mmoja kwa nafasi yake ashiriki kikamilifu katika hatua zote za maandalizi kama atakavyohitajika," alisisitiza Dk. Biteko.

Suala lingine alilosisitiza ni kwa maofisa mipango kubadilika na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi na programu zote zinazotekelezwa katika maeneo yao ikiwamo zinazofadhiliwa na wadau wa maendeleo badala ya ile inayogharamiwa na Serikali Kuu au halmashauri pekee.

Dk. Biteko pia alielekeza wakurugenzi wa mipango kuzingatia utamaduni wa kuwa na mawazo ya pamoja katika kupanga mipango ya serikali na nchi kwa ujumla ili kuleta mipango imara itakayosaidia Taifa kufikia uchumi wa juu.

Suala lingine alilosisitiza Dk. Biteko, ni wanamipango walipewa jukumu la kusimamia miradi na ufuatiliaji na tathmini; wazingatie utaratibu wa kutoa taarifa za utekelezaji programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa.

Alisema shughuli za tathmini na ufuatiliaji ni muhimu nchini, hivyo zinapaswa kupewa kipaumbele na kutengewa rasilimali za kutosha.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, aliwataka maofisa mipango kuona thamani ya kada yao na wahakikishe wanakuwa wafuatiliaji wakubwa katika upangaji wa mipango kutoka ngazi ya chini hadi Taifa kwa ajili ya manufaa ya nchi.

Pia aliagiza wakurugenzi wa sera na mipango kuweka mipango inayotekelezeka kwa manufaa ya nchi kiuchumi.

Kongamano hilo limehudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Dk. Tausi Kida na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela.

# Madereva walia urasimu uhakiki wa vyeti polisi

**Na Beatrice Shayo**

MADEREVA wa malori wamelalamikia wanachokiita "urasimu" katika uhakiki wa vyeti unaoendeshwa na Jeshi la Polisi, wakisema unasababisha usumbufu na watalazimika kupaki magari ikiwa hatua hazitachukuliwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kwa niaba ya madereva 3,000, Jumanne Sebarua, ambaye ni dereva wa masafa marefu, alisema wamekutana na changamoto ya kukamatwa na kuwekwa kituoni kisha kutakiwa kulipa faini na kuachiwa.

"Tayari madereva wameanza kukamatwa, unalipa Sh. 50,000 ili usipelekwe mahakamani. Dereva ana mzigo wa nje ya nchi analipa hiyo posho na faini ya Sh. 30,000 tunaandikiwa kuilipa.

"Sasa, tunajiuliza huu uhakiki inakuwaje tena tunapigwa faini na kuachiwa? Lengo lilikuwa faini au watu kuwa na utaalamu?" alihoji.

Dereva huyo alisema kuna haja serikali kuondoa utaratibu huo kwa kuwa wanakoelekea, watalazimika kupaki malori; si kwa lengo la kugoma, bali njia ya kusisitiza kuwekwe utaratibu ambao ni rafiki kwa madereva.

Sebarua alisema ni vizuri dereva anapokwenda kufuata leseni yake ambayo imeisha muda wake, awasilishe vyeti ndipo apewe mpya. Huo ndio utaratibu wanaoona unafaa na utasaidia kuepusha usumbufu wanaoupata kwa sasa.

"Vyuo vya kusoma vipo viwili; ni VETA na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na kwenyewe kumejaa. Tumeambiwa ni mpaka mwakani.

"Sasa utaacha kusafirisha mzigo mpaka mwakani foleni ya kusoma itakapofika? Hili jambo halijakaa sawa," alisema.

Vilevile, mwakilishi huyo wa madereva pia alizungumzia kauli ya hivi karibuni ya Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Ramadhani Ng'anzi, kwamba wanataka kuchagua dereva "pumba na mchele," akiikosoa vikali.

"Hii kauli sisi haijatufurahisha, tuna taaluma ya udereva. Tunakwenda nchi za nje na kukuza uchumi wa nchi. Kwa kifupi, tunamsaidia Rais wetu, zipo juhudi ambazo tumezifanya kama madereva.

"Kamanda anaeleza anataka madereva ambao hawana vyeti. Hata kama ana leseni wasiwe wanafanya shughuli za udereva. Hii italeta shida kubwa hasa kwenye bandari, madereva wengi wana leseni lakini hawana cheti. Amekwenda mbali hata kama una cheti hauna barua ya uhakiki bado una makosa," alilalama.

"Tunamwomba atoe tamko kama haya magari tukayapaki. Tukipaki magari wasije kusema sisi tumegoma. Hata huko vyuoni hakuna nafasi, watu ni wengi wanaotaka kusoma. Nilidhani angekuja na ile falsafa dereva ambaye hakusoma na ana leseni aende kusoma kabla ya kupatiwa leseni mpya,"alisema.

Dereva mwingine, John Thomas, alisema serikali inapaswa kuhamasisha madereva wa malori waende kusoma kabla ya leseni zao kuisha, ili wanapotaka nyingine mpya wapewe ikiambatana na cheti cha mafunzo.

"Tukisema tupaki malori huko bandarini hali itakuwaje? Au mnataka polisi waje kutukamata tuonekane tumefanya mgomo? Tanzania ni yetu, ni vizuri wakaweka utaratibu ambao ni mzuri kwa wote bila kuwapo madhara," alisema Thomas.



Waliokuwa askari wa Jeshi la Polisi, Stella Mashaka (kulia) na Majid Abdallah, wakiwa wameficha nyuso zao baada ya kutoka katika chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana kusikiliza mashtaka yanayowakabili ya wizi wa Sh. milioni 90 kwa kutumia silaha. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Kiingereza kufundishwa kuanzia darasa la kwanza shule za serikali

**Na Elizabeth Zaya**

SOMO la Kiingereza litafundishwa kuanzia darasa la kwanza kwenye shule za msingi za serikali kuanzia Januari mwakani.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Elimu), Dk. Charles Msonde aliwaambia waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam baada ya kufungua mkutano wa kimataifa wa kujadili ubora wa elimu.

"Mwakani tunaanza utekelezaji wa maboresho ya sera ya elimu kwa kuanza na darasa la kwanza kufundishwa somo la Kiingereza. Na hii sasa itasaidia kuimarisha na kuongeza uwezo kwa wanafunzi kufahamu lugha hiyo kwa ufasaha zaidi.

"Na hii itasaidia wanapomaliza elimu msingi umahiri wa lugha hiyo unakuwa mkubwa. Kwahiyo, hata wanapokuwa wanaendelea madarasa ya juu zaidi Kiingereza hakitakuwa shida tena," alisema

Dk. Msonde alisema tayari semina zimeshaanza kutolewa kwa walimu wote watakaohusika kufundisha lugha hiyo kwa wanafunzi hao wa darasa la kwanza.

"Na kwa maboresho haya ya sera ya elimu, tumepanga vitu vya kuanza kwa shule za msingi na kwa vitu vya kuanza kwa shule za sekondari, na kitakachoanza kwa shule za msingi ni maboresho ya mtaala wa elimu ya awali darasa la kwanza na la tatu, na madarasa mengine ambayo sijataja yataendelea na utaratibu wake kama kawaida,"alisema Dk. Msonde. Awali akizungumza katika mkutano huo, Rais mstaafu Jakaya Kikwete alisema kuna haja ya kuendelea kuboresha mfumo wa elimu ili uendane na kasi ya ukuaji wa teknolojia duniani.

"Dunia inabadilika na teknolojia pia nayo inakuwa kwa kasi sana kila siku na haitusubiri. Kwahiyo, na sisi tunatakiwa kuboresha mfumo wetu wa elimu ili tuendane na kasi hiyo," alisema Kikwete.

Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Ochola Wayoga, alisema miongoni mwa mambo makubwa yanayojadiliwa katika mkutano huo ni pamoja na uboreshaji wa mifumo ya elimu barani Afrika na namna inavyoakisi mapinduzi ya viwanda.

Mjadala mwingine alisema ni sera na elimu na namna teknolojia inavyosaidia ujifunzaji na upatikanaji elimu bora, aina ya walimu waliopo na namna wanavyowezeshwa.

Pia alisema watajadili uwekezaji uliopo kwenye sekta hiyo kulingana na mahitaji katika kila nchi inayoshiriki katika mkutano huo.

MIAKA 36 YA TAMWA



Ananilea Nkya



Rose Haji



Pili Mtambalike

# Waasisi wajivunia kupatikana Sheria Makosa Kujamiiana 1998

**Na Jenifer Gilla**

WAKATI Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), leo kinaanza maadhimisho ya miaka 36 tangu kianzishwe, waasisi wanajivunia kuleta mabadiliko katika mambo mbalimbali yaliyokuwa yakikandamiza wanawake, ikiwamo kuanzishwa kwa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998 (SOSPA).

Chama hicho pia kinajivunia kuvunja ukimya rushwa ya ngono kwenye vyombo vya habari, kutokomeza mauaji ya vikongwe hali iliyochangia kutengeneza jamii huru hasa ya wanawake ambao sasa wanashiriki katika shughuli za kujiletea maendeleo bila hofu.

Mmoja wa waasisi hao, Dk. Ananilea Nkya, alisema moja ya mambo makubwa ambayo chama hicho kiliyafanyia kazi na kufanikiwa ilikuwa ni kutungwa kwa Sheria ya SOSPA ambayo walianza harakati mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Alisema moja ya mikakati waliyoitumia ni kufanya utafiti ili kuonyesha ukubwa wa tatizo na athari zake kwa taifa na kushawishi mabadiliko ya sheria hiyo kwa kushirikiana na Kituo cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake (CRC).

Alisema baada ya kufanya utafiti huo waliuweka wazi kwa wananchi kupitia vyombo vya habari na taarifa ziliwafikia wanawake wengi, ndipo walipojitokeza kuwaunga mkono.

Baada ya matokeo hayo, Ananiela alisema waliingia katika mkakati wa kukusanya nguvu ya pamoja kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya vitendo hivyo kwa jamii ikiwamo kuchochea maambukizi ya Ugonjwa wa Ukosefu wa Kinga Mwilini (UKIMWI).

"Tulihakikisha tunashirikisha pia makundi yenye ushawishi kama vile viongozi wa dini, viongozi wa serikali, wasanii, taasisi binafsi kama vile TGNP, nao wakaona umuhimu wa jambo hili, wakawa sehemu ya nguvu yetu tukawa na sauti moja. Uzuri tulikuwa na watu walikuwa wameathiriwa na vitendo hivyo wakawa wanatoa ushuhuda," alisema.

Dk. Ananilea alisema hata siku ambayo mswada huo unapelekwa bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa, timu ya wanaharakati hao iliweka kambi nje ya Bunge na ulipopitishwa walishangilia kwa kuwa ilikuwa ni kitu kikubwa cha kitaifa kuwahi kutokea.

Alisema mwaka 1998 sheria hiyo ilianza kutumika rasmi na mambo mapya yaliyoongezwa ilikuwa ni ukeketaji kutambulika kama kosa la jinai, udhalilishaji wa kingono wa aina yoyote, ubakaji kupewa adhabu ya kifungo hadi cha maisha jambo lililoiamsha jamii kuheshimu haki ya wanawake.

Alisema katika harakati hizo walikumbana na changamoto mbalimbali ikiwamo mitazamo hasi kuwa wanawake ni chombo cha starehe, hivyo wakati wanafanya uhamasishaji baadhi ya watu wenye mitazamo hiyo walikuwa wanawaona kama maadui.

Pili Mtambalike, mwasisi wa chama hicho alisema miaka ya tisini iligubikwa na janga la kutisha la mauaji ya wanawake wakongwe. TAMWA walifanya utafiti kujua chanzo na zababu za mauaji hayo hasa kwenye Mkoa wa Shinyanga na moja ya majibu waliyopata ni kuamini ushirikina.

"Wanawake wazee mara nyingi ndiyo walikuwa wanashukiwa kuwa wachawi pakitokea vifo kwenye familia. Kwa hiyo walikuwa wanapigwa na kuuawa na wengi walionusurika ilibidi wakimbie makazi yao huko vijijini wahamie mjini. Shinyanga Mjini kulikuwa na kinamama wazee wengi tu wanaishi mitaani kwa kuomba omba na kwa kweli walikuwa na maisha magumu kupita kiasi," anakumbuka.

Alisema jambo lingine walilobaini katika utafiti huo ni mauaji hayo yalikuwa njia mojawapo ya kuwadhulumu wazee mali zao ikiwamo nyumba, ardhi, mifugo, vitendo vilivyokuwa vikifanywa na watu wao wa karibu.

Alisema baada ya utafiti huo walitumia kalamu zao kupaza sauti za wanawake hao. Hivyo chama hicho kilituma timu ya waandishi wa habari kufanya mahojiano na kundi hilo, jamii inayowazunguka, viongozi wa kijadi na kiserikali.

Pili alisema, baada ya habari hizo kuandikwa mafanikio yaliyopatikana yalikuwa ni kuwahifadhi kwenye makazi yao maalum na mashirika mbalimbali yalijitokeza kuwapekelea mahitaji muhimu kama nguo, chakula na ulinzi.

Alisema juhudi hizo zilizaa matunda kwa muda mfupi kwa kuwa vitendo hivyo bado vinaendelea hasa katika mikoa ya Mwanza, Geita, Kagera na kushauri waandishi chipukizi kuendelea kupaza sauti za wanawake hao ili waishi maisha wanayostahili kama walivyofanya wao.

"Ipo haja kwa vyombo vya habari hususan TAMWA ambayo uanzishaji wake ulikuwa na dhamira ya kustawisha haki za binadamu za wanawake na watoto kuendelea kupaza sauti kuhusu ukiukwaji huu mkubwa wa haki hizo," alisema Pili.

Mwasisi Rose Haji Mwalimu, anasema katika sekta ya afya, walitumia kalamu zao kuhamasisha afya salama ya uzazi na uzazi wa mpango, kwa kuelimisha jamii kuzaa watoto watakaoweza kuwatunza hali iliyochangia kupunguza vifo vya uzazi.

> **1998**
>
> Alisema mwaka 1998 sheria hiyo ilianza kutumika rasmi na mambo mapya yaliyoongezwa ilikuwa ni ukeketaji kutambulika kama kosa la jinai, udhalilishaji wa kingono wa aina yoyote, ubakaji kupewa adhabu ya kifungo hadi cha maisha jambo lililoiamsha jamii kuheshimu haki ya wanawake.

Vilevile, alisema walifanikisha kushawishi serikali kuanzisha utaratibu wa watumishi wote kuvaa vitambulisho vyenye majina yao kamili wakati wote wawapo kazini.

Alisema waandishi kutoka vyombo vya habari 15 walifanya utafiti katika zahanati, vituo vya afya, hospitali na maduka ya dawa na kubaini kuwa katika maeneo hayo kulisheheni rushwa iliyokuwa inawaathiri watu wenye vipato vya chini hasa wanawake wanapokwenda kupata huduma ya afya.

Baada ya kutoa matokeo ya utafiti huo, baadhi ya maduka ya dawa yalifutiwa leseni baada ya kugundulika kuwa zimekiuka taratibu. Serikali pia ilifanya msako dhidi ya madaktari wasiokidhi vigezo.

Hiyo ilitokana na uchunguzi wao kugundua kuwapo na wimbi la rushwa hali iliyowaathiri wanawake.

Mkurugenzi wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, alisema chama hicho kimekuwa kikipambana na rushwa ya ngono mahali pa kazi kwa kufanya utafiti na kuchapisha matokeo na madhara yake hasa kwa wanawake kupitia vyombo vya habari.

Alisema kwa miaka mitano mfululizo chama hicho kimefanya utafiti wa suala hilo katika taasisi mbalimbali ikiwamo vyuo vya elimu ya juu na vyombo vya habari kwa kushirikiana na wadau kama vile Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT-T) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU).

Alisema pamoja na juhudi hizo bado tatizo hilo lipo kwa sababu utafiti walioufanya mwaka 2021 ulionyesha kuwa asilimia 52 ya wanawake wanaopitia kadhia hiyo katika vyombo vya habari hawatoi taarifa kutokana na sababu mbalimbali.

"Katika maadhimisho ya mwaka huu TAMWA imewekeza kupinga rushwa ya ngono na unyanyasaji wa kijinsia katika maeneo ya kazi. Kwa taaluma yetu tunapinga unyanyasaji huu katika vyumba vya habari hawatoi... wanahabari, ikiwamo katika shule za habari," alisema.

# Afya ya akili yatiliwa mkazo kwa wanawake

**Na Mary Geofrey**

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amesema wanawake nchini, mbali na kujikomboa kiuchumi, wana wajibu wa kuzingatia kuchunguza tatizo la afya ya akili.

Katambi aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipofunga Mkutano Mkuu wa Jukwaa la Maofisa Watendaji Wakuu wa Wanawake Tanzania (TWCR) jijini Dar es Salaam, akimwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Alisema wanawake wana shughuli nyingi za kuwazalisha vipato na kukuza uchumi wa Taifa na katika kufikia malengo hayo, wana mambo mengi yanayowasonga yanayowasababishia msongo wa mawazo.

"Ni muhimu sana mkajikita pia kuchunguza tatizo hili kwa sababu linawaathiri watu wengi zaidi. Tatizo lingine ni kubadilisha mitizamo na kuwa na mitizamo chanya, wengi wana mitizamo hasi kwa sababu ya kushindwa kujiamini," alisema Katambi.

Alitilia mkazo kuwa wanawake wanatakiwa kujitambua, kujiwekea malengo, kuwa na maadili, nidhamu, vyote vitasaidia kuendelea kupiga hatua ya maisha na kiuchumi.

Aliwataka pia kuwekeza kwenye teknolojia kwa sababu wakiitumia vizuri itawasaidia kufungua mipaka na kuitumia kuwakuza kibiashara.

Awali akisoma hotuba ya Majaliwa, Katambi aliagiza kuimarishwa kwa kanzidata ya viongozi na maofisa watendaji wakuu wanawake katika sekta ya umma na binafsi kwa ajili ya kupata taarifa.

Kwa mujibu wa Majaliwa lengo ni kupima shabaha na viashiria ili kupata takwimu zilizo sahihi kwa maendeleo na maslahi mapana ya Taifa.

Katiba hotuba yake hiyo, Majaliwa pia aliagiza Bodi ya Wakurugenzi TWRC itafute namna ya kushirikiana kwa karibu Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) ili kubaini maeneo yenye uhitaji kwa ajili ya kuandaa programu za kujenga uwezo.

Awali Mwasisi wa TWCR, Emma Kawawa, aliomba serikali kuyatafutia ufumbuzi matatizo yanayowakabili ikiwamo kushindwa kushiriki shughuli za maendeleo kama miradi ya kimkakati.

Alisema pia ukosefu wa vifaa vya kutosha na ukosefu wa ujuzi kwa baadhi ya wanawake wakurugenzi katika kutekeleza majukumu yao ni miongoni mwa mambo yanayowasumbua.



Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, Hamis Taletale maarufu Babu Tale (kushoto), akikabidhi gari la wagonjwa la Hospitali ya Tarafa ya Mkuyuni kwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Lucas Lemomo (kulia), katikati ni Mganga Mkuu wa Kituo cha Afya cha Mkuyuni, Dk. Antony Dilima. **PICHA NA ASHTON BALAIGWA,MOROGORO.**

# Wenye majeraha ya moto na ajali kurekebishwa maumbile

**Romana Mallya**

MADAKTARI bingwa kutoka Hospitali ya Aga Khan, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na wataalamu wengine kutoka Ulaya na Marekani, leo wanaanza upasuaji wa kurekebisha maumbile yakiwamo majeraha makubwa yatokanayo na moto kwa wanawake na wasichana 25 bila malipo.

Upasuaji huo ambao unafanyika katika Hospitali ya Aga Khan kwa siku tano kuanzia leo, utashirikisha pia madaktari kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Ziwa (Bugando) na Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, Zanzibar ili kujengewa uwezo katika eneo hilo.

Wengine watakaofanyiwa ni wenye kasoro kubwa za kimwili, waathirika wa ukatili wa kijinsia na wale waliokatwa titi au matiti baada ya kugundulika kuwa na saratani kutengenezewa mwonekano mpya.

Daktari Mwandamizi wa Upasuaji na Mkuu wa Idara ya Upasuaji katika Hospitali ya Aga Khan, Dar es Salaam, Athar Ali alisema jana kuwa programu hiyo inalenga kurejesha utendaji wa kimwili ili kuwezesha na kuboresha maisha ya wanawake na wasichana wa Tanzania.

"Katika awamu saba zilizopita kati ya mwaka 2016 na 2022, wataalamu 16 wakiwamo madaktari wa upasuaji wa kurekebisha maumbile, madaktari wa upasuaji wa kawaida na madaktari wanafunzi kutoka hospitali za umma kama Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Bugando, Hospitali ya Mnazi Mmoja - Zanzibar, Hospitali ya Aga Khan - Dar es Salaam wamepata mafunzo kupitia programu hii," alisema.

Daktari Bingwa wa Upasuaji na Kiongozi wa Timu ya Reconstructive Women International, Andrea Pusic, alisema huu ni mwaka wa nane wa ubia na Hospitali ya Aga Khan, Dar es Salaam na Hospitali ya Taifa Muhimbili katika eneo hilo.

Alisema ushirikiano huo umeleta ongezeko kubwa la utaalamu na uwezo wa madaktari wa upasuaji kurekebisha maumbile.

"Kwa pamoja tumeweza kuhudumia mamia ya wanawake na wasichana waliojeruhiwa ili kuboresha utendaji wa kimwili na mwonekano wao," alisema.

Daktari Bingwa wa Upasuaji katika Hospitali ya Aga Khan, Aidan Njau, alisema upasuaji huo unahusisha wagonjwa kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania wenye changamoto kubwa kama vile majeraha ya moto na ajali yaliyosababisha sehemu za miili yao kuharibika vibaya.

"Programu hii ya siku tano itawasaidia hasa wanawake na wasichana, kwa kuwa hili ndilo kundi linaloathiriwa zaidi na changamoto hizi.

"Kwa sababu ya wahisani waliojitolea kuendesha programu hii, uchunguzi na matibabu yanatolewa bila gharama yoyote. "Programu hii inaendeshwa kila mwaka na madaktari bingwa kutoka Ulaya na Marekani na kila mwaka tunapata ushirikiano na shauku kubwa kutoka kwa Watanzania," alisema.

Dk. Njau aliwakumbusha Watanzania kutumia fursa ya matibabu hayo ambayo kwa kawaida ni ghali, lakini sasa yanapatikana bila malipo.

Alisema mpaka sasa kwa kushirikiana na wataalamu wa nje, wameweza kupata utaalamu na kuurithi na kutoa kwa jamii.

"Ninaiasa jamii hawa watu msiwaficheni ndani, matibabu yapo na ni bure hapa na mnaposikia hizi nafasi waleteni wapate huduma ya utaalamu wa hali ya juu," alisema.

Mkuu wa Upasuaji wa Kurekebisha Maumbile katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Edwin Mrema, alisema, "sisi kama madaktari wa upasuaji wa kurekebisha maumbile, wasaa wa kuridhisha zaidi katika kazi yetu ni pale tunaposaidia kurejesha tabasamu na hali ya kujiamini iliyopotea kwa wanawake na watoto."

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Aga Khan, Sisawo Konteh, aliwashukuru wahisani kwa michango yao mikubwa ya kifedha kwa ajili ya kuunga mkono upasuaji huo kwa miaka mingi. Konteh alitaja baadhi ya mambo waliyojifunza katika miaka iliyopita, ikiwamo kushirikiana na Taasisi ya Lady Fatemah Trust kuongeza usaidizi wa afya ya akili kwa wagonjwa baada ya kufanyiwa upasuaji ili kukidhi mahitaji yao ya kisaikolojia na kuwasaidia kurejea katika maisha yao ya kawaida.

Kwa mujibu wa wataalamu hao, mgonjwa mmoja anayekwenda nje kutibiwa matatizo hayo hutumia mpaka Sh. milioni 50 na akirejea nyumbani, vidonda vikaleta shida, analazimika kutibiwa tena na wataalamu wa ndani.

Awali zaidi ya wanawake na wasichana 60 wenye matatizo yanayohusiana na majeraha ya moto na wanaosumbuliwa na changamoto za ukatili kutoka sehemu mbalimbali Tanzania walifanyiwa uchunguzi bila gharama yoyote, ikiwamo uchunguzi uliofanyika Zanzibar.

Baadaye wanawake 25 na wasichana saba walichujwa kwa ajili ya uchunguzi zaidi ili kubaini ustahiki wao wa kufanyiwa upasuaji ndipo walipopatikana 25 waliokidhi vigezo vya kurekebishwa maumbile.

# Mbaroni kwa tuhuma kukata vichwa mama na mwanawe

**Na Waandishi Wetu,**
MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro limemtia mbaroni Selemani Sita (25), mkazi wa Seke mkoani Mwanza kwa tuhuma za mauaji ya mama na mtoto wake wilayani Ulanga mkoani Morogoro kwa kuwakata vichwa na kuondoka navyo.

Inadaiwa mtuhumiwa huyo alikamatwa akiwa kwenye harakati za kutoroka kwa kutumia usafiri wa basi la abiria lililokuwa linaelekea Bukoba, mkoani Kagera.

Kamanda wa Polisi mkoani Morogoro, Alex Mkama alisema jana mjini hapa kuwa mtuhumiwa huyo anadaiwa kufanya mauaji hayo ya kikatili Novemba 24, mwaka huu katika Kitongoji cha Ilangali, Kijiji cha Mavimba, Kata ya Milola, wilayani Ulanga.

Mkama alisema mtuhumiwa baada ya kukamatwa akiwa kwenye basi la abiria lililokuwa linaelekea Bukoba, alikwenda kuonesha askari polisi alikotupa vichwa hivyo.

"Tunaendelea na uchunguzi na muda wowote utakapokamilika hatua zingine za kisheria zitafuata," alisema Kamanda Mkama.

Katika tukio hilo, Mwanaisha Matele (37) na mwanawe Baraka Maita (7), wakazi wa Kijiji cha Mavimba, waliuawa kwa kuchinjwa, kichwa kikitenganishwa na kiwiliwili na mtu ambaye hakufahamika. Aliondoka na vichwa vyao.

Mwanaisha na mwanawe Baraka ambaye alikuwa mwanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Mavimba walikutwa na umauti huo kwa kutendwa ukatili na mtu aliyekaribishwa nyumbani kwao, wakiishi naye kwa wiki mbili.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mavimba Salehe Ndopi, alisema tukio lilitokea Novemba 24 mwaka huu saa majira ya 12 asubuhi huko Kitongoji cha Ilangali, likiibua mshangao na simanzi kijijini mwake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TAMWA ina kila sababu kujivunia miaka 36

**CHAMA** cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), leo kinaanza maadhimisho ya siku mbili ya miaka 36 tangu kilipoanzishwa na mgeni rasmi katika kilele ambacho kitafanyika Novemba 29, anatarajiwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

TAMWA ilianzishwa kwa madhumuni ya kutetea haki za wanawake na watoto na katika hilo imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuwakomboa kutoka katika ukandamizaji na sasa wakati kikisherehekea miaka hiyo kinajivunia kuona wanawake wengi wakiwa katika nafasi za juu za uongozi.

Wanawake na watoto walikuwa wakipitia udhalilishaji na ukandamizaji na hawakujua pa kukimbilia, lakini TAMWA ilifanikiwa kuwakomboa kupitia elimu ya kutambua haki zao ya kutoa taarifa kila wanapokutwa na madhira hayo.

Katika moja ya mafanikio makubwa ambayo chama hicho inajivunia ni kupatikana kwa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA), ambayo inatoa adhabu kali kwa watu wanaofanya udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto.

Wanaharakati walijitoa kwa kupiga kambi nje ya ukumbi wa Bunge, Dodoma, kwa kulala kwenye mahema bila kujali baridi wakihamasisha Wabunge kupitisha muswada wa sheria hiyo ili iweze kufanyakazi.

Pamoja na juhudi hizo TAMWA imewajengea uwezo wanawake wengi ambao hapo mwanzo walikuwa wakiogopa kujitokeza kugombea nafasi za uongozi kutokana na mfumo dume uliojengeka.

Kupitia elimu waliyoitoa kwa njia ya uhamasishaji na mafunzo, wanawake wengi walitambua haki zao na kupata mwamko wa kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi zikiwamo za siasa na mpaka sasa tunashuhudia wabunge wanawake wakiongezeka bungeni.

Mafanikio haya ya TAMWA yamechangiwa pia na asasi mbalimbali zilizokuwa zikishirikiana nazo katika mapambano ya kutafuta haki za wanawake na watoto.

Waasisi wa chama hicho, walifanya kazi kubwa ya kukianzisha chama hicho ambacho kilikuwa kikibezwa na kuitwa chama cha watu walioachwa na waume zao au chama cha wanawake wasiokuwa na waume, lakini pamoja na kejeli hizo walisimama kidete hawakujali kashfa na chama kilisimama, watoto na wanawake wakaanza kupiganiwa haki zao.

TAMWA sasa inatambulika kitaifa na kimataifa kutokana na juhudi zake kubwa inazofanya za kumkomboa mwanamke na mtoto. Umaarufu wake unajulikana kiasi cha jamii inapoona uonevu ukifanyika kwa mwanamke huambiwa nenda TAMWA utapata haki yako.

Wanawake wengi walikuwa wakidhulumiwa mali zao baada ya kufiwa na wenza wao na kufukuzwa na watoto kama mbwa, lakini TAMWA ambayo pia ilianzisha kitengo chake cha kutoa msaada wa kisheria kimewasadia kinamama wengi kupata haki zao na sasa wanaishi maisha yenye furaha.

Baadhi ya waasisi wa chama hicho waliopambana kuhakikisha kinasimama na kutimiza lengo la kuanzishwa kwake, wameshatangulia mbele za haki, akiwamo marehemu Leila Sheikh na Jamillah Chipo. Mungu aendelee kuwapa pumziko la amani kwasababu wameacha alama kubwa kwenye chama na mchango wao mpaka leo unatambulika.

Ni jukumu la wanahabari wote, wakiwamo wanaume ambao pia wamejengewa uwezo na TAMWA katika kuibua habari za ukatili wa kijinsia kujivunia mafanikio hayo kwa kusherehekea maadhimisho haya kwa ushiriki mzuri wenye kuleta tija kwa jamii.

Hongereni TAMWA, hongereni wanahabari wote mliokuwa kwenye mapambano ya kupinga vitendo vya ukatili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Tuntule Swebe

# Utafiti unusuru watoto hawa

**JAMII** ya sasa inashangaza kwa mengi mojawapo linalotia fora ni kutowajali watoto, ambao wanaishi na kukulia barabarani.

Ni simanzi kwa watoto hawa na taifa lakini kwa kizazi kijacho zaidi, kwa vile wapo baadhi ya Watanzania hawa wadogo ambao wamekulia na kuishi mitaani bila malezi bora, huduma za msingi wala uangalizi wa mzazi au mlezi.

Ndiyo maisha yao, hawana chakula, pakulala, hawaendi shule na cha ajabu tena cha chakusikitisha ni watoto ambao huzurura kila kona na maskani ya wengi ni masokoni.

Huko wanalala hata barabarani na imekuwa ni kawaida kuona wimbi kubwa la watoto likiongezeka lakini hakuna juhudi za kulipatia ufumbuzi suala hilo.

Ni nyakati kama hizi mvua zinanyesha hawana makazi, malazi wala mavazi, chakula wala msaada na inawezekana wengine wanaumwa maradhi mfano homa za matumbo na nyumoni hivi najiuliza ni nani wa kuwatazama?

Ikumbukwe kuwa kifo hakikwepeki watoto wa wanaoishi kwenye mazingira magumu nao huumwa na kufa pia kwa kukosa msaada serikali na wadau ni wakati wa kuinuka na kuwasaidia, siyo kuachia mambo yabaki kama yalivyo.

Tena jamii isijisahau kuwa kwenye kundi la watoto hawa wapo wanaoishi na ulemavu mfano mara nyingi wanaonekana Tegeta kwa Ndevu na hata Mwenge Dar es Salaam.

Wanaoishi kwenye mazingira magumu wanaonekana kwenye barabara nyingi ambazo hutumiwa na viongozi, ukweli ni huu watoto hawa wapo kwenye maeneo mengi hapa jijini na majiji mengine kama Mwanza, Arusha, Mbeya na Dodoma.

Wakati umefika kujiuliza je chanzo cha watoto hawa kukimbilia mitaani ni nini hasa? Aidha, ifanyike pia sensa wajulikane ni wangapi na uchunguzi ufanywe kufahamu taarifa wazazi na walezi wao.

Ikumbukwe kuwa kuna watoto watukutu wanaokimbia majukumu ya nyumbani na kuwaacha wazazi na walezi wakihangaika kuwatafuta bila kujua taarifa zao.

Lakini, katika hili tusisahau walezi wengine hawana maadili wana mienendo isiyokuwa na hekima na misimamo mema, huwanyanyasa, kuwanajisi na kuwaumiza watoto na huenda kikawa chanzo cha kukimbia nyumbani kwao.

Upo pia ukatili unaohusisha vipigo vinavyopitiliza, kuteswa kwa sababu pengine ndogondogo kama kula mboga iliyokusudiwa kutumika usiku , kupoteza hela, kushindwa kupika na hata kushindwa kufanya kazi kwa kasi.

Pia, serikali kwa kushirikiana na mashirika ya kiraia, iangalie uwezekano wa kufanya utafiti kwenye masuala ya kutumikisha watoto kwenye ajira haramu kwenye mashamba, kuchimba madini na hata ufugaji yote hayo yakichangia kutoroka na kukimbilia mijini.

Utafiti unahitajika kwa kuangalia ukweli kuwa baadhi hudanganya wazazi, walezi na watoto kuwa wanawapeleka kwenye masomo au kuwaendeleza kiufundi lakini ni udanganyifu na matokeo yake huwachukua na kuwaingiza kwenye madanguro na baa mijini, yote hayo yakifanywa kupitia usafirishaji haramu wa binadamu.

Utafiti ukifanyika utagundua kuwa nini kinafaa kuwa ufumbuzi ili kuondoa changamoto inayolikabili kundi hilo la watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Halikadhalika kuna baadhi ya wasichana wanaokimbia kulazimishwa ndoa za utotoni, kutumikishwa na kufanyishwa kazi ambazo ni ngumu na zinazoumiza wato.

Inawezekana ni nyumbani kwa watu kuwa watumishi wa ndani, pengine hawalipwi ujira na fedha zao huchukua mama aliyemfikisha kwa mwajiri.

Kuna wengine hufanyishwa kazi za mashambani kulima, kupalilia, kununyuzia mimea kemikali za kuua wadudu na kuvuna kwaujira mdogo tena bila chakula japo kazi hizo huchosha na kuumiza mwili.

Lakini, utafiti ukifanyika utatoa jibu maana upo usafirishaji haramu wa binadamu unaotoa watoto nyumbani kwao na kuwaleta mijini kwa ahadi za kusomeshwa , kupewa kazi nzuri kumbe si kweli wanapelekwa kwenye madanguro au kuuza baa.

Baadhi hukimbia na kuanza maisha mitaani hivyo utafiti huo ni jibu na ndiyo utakaotoa mwanga wa nini cha kufanya.

## HABARI KITAIFA

# Wananchi Mkuyuni wapatiwa gari la wagonjwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WANANCHI wa Tarafa ya Mkuyuni, Wilaya ya Morogoro, mkoani hapa, waliokuwa wakisafirisha wagonjwa kwa gharama ya Sh. 70,000 hadi Sh. 100,000 kwenda hospitali ya rufani, sasa wamepatiwa gari la wagonjwa.

Pia, wataondokana na tishio la vifo vya wajawazito na watoto baada ya serikali kufanya uwekezaji katika sekta ya afya, ikiwamo huduma za upasuaji na matibabu ya dharura katika Kituo cha Afya Tarafa cha Mkuyuni.

Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, Hamis Taletale (Babu Tale), akikabidhi gari hilo kwa Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk Antony Dilima, alisema litaleta ukombozi kwa wagonjwa.

Dk. Dilima alisema, limekuja kama neema kubwa kwa wagonjwa ambao watahitaji kupata huduma za ziada kusafirishwa umbali wa kilomita 50 hadi kufikia Hospitali ya Rufani Morogoro.

"Pale ambapo anapokuja mgonjwa na tunapoona huduma hizo sisi hatuzitoi tunamwandikia aende hospitali ya rufaa ya Morogoro na sisi tulikuwa hatuna gari hapa hivyo analazimika kukodisha gari lolote," alisema Dk. Dilima.

Kuhusu uboreshwaji wa huduma za afya, alisema uwekezaji huo umesaidia kuokoa vifo vya wajawazito na watoto 33 kila mwezi.

Zainabu Athumani, mkazi wa Mkuyuni, alisema wakati akiwa mjamzito mwaka jana, alilazimika kukodisha gari kwa Sh. 80,000 kupelekwa Hospitali ya Rufani Morogoro kwa ajili ya kwenda kufanyiwa upasuaji na kupatikana kwa gari hilo kutawasaidia kinamama na watoto.

Mbunge Taletale, alisema anamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumpa kipaumbele kwa kuwa kati ya magari ya wagonjwa 200 yaliyotolewa na Rais, yeye ni mmoja wa wanufaika.

"Asitokee mtu akaja kuwaongopea hapa kuwa anapendwa na Rais, ni muongo tu huyo embu tujiulize kuna wabunge wangapi hapa nchini? Lakini kati ya magari ya wagonjwa 50 yaliyotoka kati ya 200 yaliyoletwa mimi nimepewa kipaumbele ndio hili hapa nimelileta," alisema.

Alisema amefurahi kutimiza ahadi yake aliyoitoa kwa wakazi wa tarafa ya Mkuyuni na hivi sasa ni kusimamia ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami kutoka Bigwa-Kisaki ambayo itaanza muda wowote baada ya mkandarasi kupatikana.

"Wote mmemsikia Waziri wa Ujenzi hapa baada ya kumpigia simu, ameshasema tayari mkandarasi ameshapatikana na ujenzi wa barabara ya Bigwa-Kisaki utaanza wakati wowote kuanzia sasa, mnataka nini tena wana Mkuyuni," alisema Mbunge Taletale.



Mfanyabiashara mdogo akiwa amebeba meza yake na kuipeleka katika eneo analofanyia biashara Mbezi Mwisho Dar es Salaam juzi. Baada ya kumaliza biashara jioni mara nyingi huziondoa meza hizo wakihofia kubomolewa na mgambo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Daktari: Using'oe jino unaongeza vibogoyo, mashavu kuporomoka

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Msaidizi Huduma za Afya ya Kinywa na Meno kutoka Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, amesema jino linalouma halipaswi kung'olewa akisema hiyo ni hatua ya mwisho, kwa kuwa kiungo hicho ni muhimu kama kingine mwilini.

Alisema jino linapaswa kutibiwa na si kung'olewa kwa kuwa wizara hiyo imebaini wengi wanaong'olewa meno ni sababu ya kukosa gharama za tiba na baadhi ya mabingwa kuona uvivu kulitibu.

Daktari Nzobo, aliyasema hayo hivi karibuni jijini Tanga katika mkutano uliowakutanisha Chama cha Wataalam wa Afya ya Kinywa na Meno Tanzania (TDA), na kufunguliwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

Alifafanua namna dhana ya dawa ya jino ni kuling'oa, inavyoathiri jamii akitoa wito wa umma kuachana nayo, kutokana na kukua kwa teknolojia ya matibabu eneo hilo, inayotoa mazingira rafiki ya kulitibu jino badala ya kung'olewa.

"Ukienda hospitali utafanyiwa matibabu kulingana na teknolojia ilivyokua. Suluhu ya mwisho kama vile mtu anayekatwa mguu huwa ni ya mwisho wakati tiba za awali zimeshindikana, hii ni kama vile kuling'oa jino iwe ni hatua ya mwisho, sio jino likiuma, limetoboka linaondolewa hiki ni kiungo muhimu mwilini kama vingine.

"Jino halipaswi kuondolewa. Wenzetu wameanza teknolojia ya kulitibu jino siku nyingi. Jino hata liume namna gani halipaswi kuondolewa, linapaswa litibiwe na uendelee kulitumia jino lako. Kuna tiba ya mizizi kama limetoboka, na utalitumia maisha yako yote yaliyobaki, labda liwe limeharibika vibaya mno," alisema Dk. Nzobo.

Alisema kilichopo ni kuwapo kwa gharama za matibabu ambazo wengi hawazimudu, ili kuepukana na maumivu hufikia hatua ya kuling'oa, huku akishauri Watanzania wajiunge na Bima ya Afya kwa Wote, kuepukana na gharama hizo.

"Tunawashauri wananchi wajiunge na bima ya afya, itasaidia kwenda hospitali kupata matibabu bure. Sababu za jino kutoboka, kuuma ni mabaki ya chakula na kutengeneza tindikali."

Dk. Nzobo anashauri watu wapige mswaki angalau mara mbili kwa siku, yaani asubuhi na jioni ama usiku kabla ya kulala, kuondoa mabaki ya chakula ambayo yanasababisha jino kuharibika.


Alisema wito kwa wananchi kutokuwa wepesi kuling'oa jino kabla ya tiba, akisema mabingwa wa kinywa na meno wana utaalamu wa kufanya tiba.

"Daktari anayekimbilia kuling'oa jino ni mvivu. Hospitali binafsi, umma wananchi msikubali kung'olewa jino haraka. Wataalam walipo maeneo ya kutolea tiba wamefundishwa. Msimamo wa serikali kwa sasa ni huo, itolewe tiba.

"Unapoondoa jino unaongeza idadi ya watu vibogoyo, uso unazeeka au mashavu kuporomoka na mwonekano unakuwa sio mzuri usoni," alisema Dk. Nzobo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Waliovamia kongani za malisho mifugo wapewa siku 7 waondoke

**Na Paul Mabeja,** KITETO

SERIKALI imetoa siku saba za kuondoka watu wote waliovamia na kufanya shughuli za kilimo kwenye maeneo ya kongani za malisho ya mifugo zilizotegwa kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi za vijiji wilayani Kiteto mkoani Manyara.

Watakaokaidi agizo hilo baada ya muda huo, itaendeshwa operesheni ya kuwaondoa kwa nguvu watu wote waliovamia maeneo hayo na kuwafikisha mahakamani.

Mkurugenzi Msaidizi wa Uendelezaji Maeneo ya Malisho Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Gabriel Bura alitoa maagizo hayo juzi wakati wa kikao cha viongozi wa kimila wa jamii ya Kimasai na Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) kilichofanyika wilayani hapa.

Bura alisema maeneo hayo ya kongani za malisho kwa ajili ya mifugo yalitengwa kwa mujibu wa sheria, hivyo watu wote ambao wamevamia hivi sasa na kufanya shughuli nyingine tofauti na ufugaji wanatakiwa kuondoka mara moja.

"Ninatoa siku saba watu wote wawe wameondoka kwani maeneo yale yametengwa kwa ajili ya ufugaji tu na si kitu kingine na kwa yule ambaye atafanya shughuli nyingine zaidi ya ufugaji anavunja sheria.

"Mpango wa matumizi bora ya ardhi nchini umefanyika kwa asilimia 45 na maeneo ambayo yametekeleza zaidi ni Manyara na Arusha. Hapa kwenu mpango umefanyika ni jukumu lenu kuzilinda hizi kongani za malisho. Sheria ya Malisho inakataza maeneo haya mtu kulima, kujenga au kuchimba madini," alisisitiza.

Alisema kuwa katika kipindi hicho cha siku saba, watu wote wanapaswa kuondoka bila kujali ni wafugaji au wakulima.

"Nitoe wiki moja viongozi wote wanaofanya shughuli yoyote ambayo haihusiki kisheria watoke kwani wote ni wavamizi bila kujali walikotoka.

"Pia niwaombe ninyi wafugaji kuwa walinzi wa maeneo haya kwani ninyi ndio mmekuwa mnawakaribisha watu kwenye hizi kongani za malisho," aliagiza.

Mwenyekiti wa Malaigwanani (viongozi wa kimila wa kabila hilo) Wilaya ya Kiteto, Emmanuel Sinogoro, aliomba serikali kuchukulia hatua za kisheria dhidi ya baadhi ya wafugaji waliokaidi agizo la kutoka kwenye maeneo ya nyanda za malisho.

Alisema hali hiyo itasaidia kuondokana na kero ya maeneo ya malisho katika wilaya hiyo inayosababisha migogoro ya muda mrefu baina ya wafugaji na wakulima.

Sinogoro alisema kuwa moja ya sababu zinazochangia maeneo ya malisho kuvamiwa ni wafugaji wenyewe kukaribisha watu kwa ajili ya shughuli za kilimo kwenye kongani za malisho.

"Hivyo basi, tunaomba iundwe timu iende kubaini watu wote walivamia ili waondolewe kama ambavyo tulikubaliana sisi wafugaji tuwe wa kwanza kuachia maeneo hayo yalitotengwa kwa ajili ya kongani za malisho," alisisitiza.

Makamu Mwenyekiti wa CCWT, Kusundwa Wamalwa, alisema kuwa baada ya kipindi hicho cha siku saba, wataziomba mamlaka husika kuchukua hatua kali kwa wataokaidi agizo hilo.

Alisema ili jamii ya wafugaji nchini ipate mafanikio inapaswa kushirikiana kwa kila jambo ikiwamo kupinga vitendo vya unyanyanyasaji vinavyofanywa na baadhi ya viongozi wa serikali na askari wa mapori ya akiba nchini.



Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Oryx Gas Tanzania, Benoit Araman, wakibadilishana mikataba baada ya utiaji saini hati ya makubaliano ya ushirikiano jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DAWASA yajiunga na e-GA kuboresha huduma zake

**Na Joseph Mwendapole**

KATIKA jitihada za kuboresha utoaji huduma za majisafi kwa njia ya mtandao, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imejiunga na mifumo mbalimbali ya pamoja inayoratibiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

Hatua hiyo imefikiwa ikiwa ni sehemu ya utekelezaji maagizo ya serikali ya kuzitaka taasisi za serikali kutekeleza sheria iliyoanzishwa Serikali Mtandao kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa umma.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia na Mawasiliano (TEHAMA) wa mamlaka hiyo, Charles Kayuza alisema jana kuwa wanalenga kuboresha njia za utoaji huduma kwa wananchi hususani huduma zinazopatikana kwa njia ya mtandao.

Alisema mamlaka itanufaika na mifumo hiyo ya TEHAMA kwa kuwa usalama wa mifumo ni wa uhakika na utasaidia kuchochea ufanisi katika kutoa huduma ya maji kwa wateja.

Aliitaja mifumo mbalimbali inayotumika kuwa ni pamoja na Maji's, NeST, ERMS, GMS na E-office ambayo inafikika kwa uhakika na usalama, hivyo kujiweka mbali dhidi ya wahalifu wa mtandao na hatari nyingine.

"Kwa sasa teknolojia imekua na kuleta mabadiliko makubwa, hivyo ni vyema kutumia mifumo yenye usalama wa hali ya juu ili kuboresha huduma kwa wateja. Pia kunakuwa na uhakika wa upatikanaji mifumo muda wote," alisema.

Kayuza aliongeza kuwa DAWASA kupitia watumishi wa TEHAMA itanufaika kwa kupata ujuzi mkubwa wa namna ya kuendesha mifumo hiyo kwa ufanisi na kwa ubora ili kuboresha upatikanaji huduma kwa wananchi wote.

# RC Chalamila azipa jukumu SACCOS miradi ya uwekezaji

**Na Christina Mwakangale**

MKUU wa Mkoa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amevitaka Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) viwe na ubunifu kwa kuwekeza katika miradi yenye tija na kutimiza haki ya mikopo kwa wanachama.

Alielekeza hayo jana mwishoni mwa wiki alipozindua matumizi ya kadi ya kibenki (VISA maalum) kwa ajili ya kutolea fedha kwenye mkutano mkuu wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO-SACCOS), mkoani Dar es Salaam.

"Nimeelezwa kwamba utendaji wa chama (SACCOS) umeimarika zaidi kwani hisa za wanachama, mtaji na mikopo ya wanachama vimeongezeka licha ya changamoto ya kupungua kwa idadi ya wanachama na ukwasi.

"Kuimarika kwa wigo wa kukopesheka kwa wanachama kumesababisha utoaji huduma za mikopo kuwa wa foleni na kusababisha wanachama kutofikia malengo ya mikopo waliyoomba," alisema.

Chalamila alisema pamoja na changamoto hiyo, bado kuna faida inayoonekana na imeongezeka kulinganishwa na mwaka ulioishia 2021. Mafanikio yanonesha kuwapo utendaji bora na ubunifu wa viongozi ikiwamo bodi ya chama hicho.

"Ninawapongeza sana TANESCO-SACCOS kwa uthubutu mlio nao wa matumizi ya TEHAMA katika utendaji kazi wenu. Sote tunajua faida za matumizi ya TEHAMA, na nitoe rai kwenu kupeleka mwamko huu hata kwa wanaushirika wengine kwa maendeleo ya nchi yetu.

"Nitoe rai kwa bodi ya chama kuhakikisha malengo mliyojiwekea katika mpango, yanatekelezwa kwa ufanisi mkubwa kama ilivyotarajiwa sambamba na kuratibu maandalizi ya mpango mkakati mpya wa tatu wa mwaka 2024 hadi 2028," aliagiza.

Awali Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO-SACCOS, Somoe Nguhe alisema akiba ya chama hicho imekua kutoka Sh. bilioni 41.9 mwaka 2022 na kufikia Sh. bilioni 44.1 kwa sasa, sawa na ongezeko la asilimia 5.2.

Vilevile, Somoe alisema kiwango cha mtaji kimekuwa na kufikia Sh. bilioni 2.9 mwaka 2022 kutoka Sh. bilioni 2.4 kwa mwaka 2021, ikiwa ni ongezeko la asilimia 22.7.

Collins Nyakunga, Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika Usimamizi na Udhibiti, alisema kuna haja ya vyama vingine kujifunza hatua iliyofikiwa na chama hicho, ikiwamo kuwa na kadi ya kieletroniki ya kufanya miamala ya kifedha.

Alisema dosari katika usharika wowote huwapo. Unapaswa kufanyiwa kazi, akimpongeza Mwenyekiti wa SACCOS hiyo kwa usimamizi madhubuti.

"Ubunifu wa chama unasaidia kukuza chama hususan kuboresha maisha ya wanachama kutokana na umoja. Muhimu kuwapatia wanachama mikopo ndani ya muda mfupi pale wanapoomba kwa sababu awali vyama kadhaa vilikuwa vinachukua muda mrefu.

# Mbowe awasihi maaskofu wahubiri haki

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amewasihi maaskofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kutojitenga na kazi ya kuhubiri haki hadi taifa litakapokaa sawa.

Akizungumza juzi katika harambee ya kuchangia ujenzi wa jengo la Usharika wa Ilkiranyi wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini Kati, Mbowe alisema kuwa kama maaskofu wangetambua heshima na thamani wanayopewa na waumini wa kanisa hilo, wangewaonya wanasiasa na kuwaelekeza namna gani ya kuishi maisha ya haki katika taifa.

"Mimi nimekuwa nikiizungumzia haki kila mahali, nikikutana na Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan), namuambia kuhusu haki. Nikikutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa) ninamwambia, lakini nikikutana pia na wananchi, naihubiri haki mpaka nitakapoona taifa limekaa sawa.

"Laiti mngejua heshima na utukufu tunaowapa nyinyi maaskofu, mngetukemea, kutuonya na kutuelekeza namna gani ya kuishi maisha ya haki katika taifa letu, ili tuweze kupata kizazi chenye kuitenda haki."



Kwa mujibu wa Mbowe, viongozi wa dini ni sauti ya Mungu, hivyo hawapaswi kujitenga na jukumu la msingi la kuhubiri haki ambayo ni zao la amani katika taifa.

Alisema wakati mwingine dunia inafika pabaya siyo kwa sababu ya watu wake kuwa wabaya, bali ni kwa sababu ya wale watu wema walioamua kukaa kimya bila kusema wema huo.

Katika harambee hiyo, Mbowe, aliahidi kuchangia Shilingi milioni 25 kati ya Shilingi milioni 200 zilizochangwa na waumini wa Usharika wa Ilkiranyi.

Awali katika ibada maalumu iliyofanyika usharikani hapo, Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini Kati, Dk. Solomon Masangwa, alisema viongozi wa upinzani nchini wanasaidia kurekebisha mambo kukaa sawa kwenye taifa.

"Haimaniishi kuwa mnapoitwa wapinzani, kazi yenu ni kupinga kila kitu hapana. Nyinyi mnasaidia taifa kujirekebisha pale linapoona limeenda vibaya kwa kupitia kuzungumza kwenu na kukosoa kwenu, hivyo nyinyi siyo wapinzani tu," alisema Dk. Masangwa.

## TRA yajivunia kukusanya mabilioni bila mabavu

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKOA wa Manyara umevuka lengo kwa kukusanya mapato ya serikali zaidi ya Shilingi bilioni 4.9 katika kipindi cha miezi minne.

Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Mapato (TRA), mkoani hapa, Shufaa Mukhandi, alisema kiasi hicho ambacho ni sawa na asilimia 113 wamekusanya kati ya Julai hadi Oktoba mwaka huu kutoka kwa wafanyabiashara bila ya kutumia nguvu kama ilivyokuwa ikifanya awali.

Akizungumza jana mjini Babati wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Shukrani kwa Mlipakodi Mukhandi, alisema makusanyo hayo ni makubwa ikilinganishwa na ya mwaka wa fedha 2022/23 ya Shilingi bilioni 38.3 sawa asilimia 114.6.

"Walipakodi wamekuwa na mchango mkubwa na maono ya Rais (Samia Suluhu Hassan) ndio yametusaidia kukusanya kodi ya serikali vizuri na wafanyabiashara wakatuelewa," alisema Mukhandi.

Awali akizindua wiki hiyo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Babati, Halfan Matipula, aliwapongeza TRA kwa kutekeleza falsafa ya Rais Samia ya kutotumia mabavu.

"Sisi tunaopitia taarifa za makusanyo kila mwezi tunaona trendi ya ukusanyaji inavuka asilimia 100 kila mwezi mnayo sababu ya kumshukuru mlipakodi kwa kulipa vizuri," alisema Matipula.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Manyara, Musa Msuya, alisema wateja wao hawajalalamika kuhusu matumizi ya nguvu wakati wa ukusanyaji kodi ya mapato.

Ofisa Elimu na Huduma kwa Mlipakodi wa TRA Mkoa wa Manyara, Serapio Luanda, alisema kuzinduliwa kwa wiki hiyo kutakuwa na mfululizo wa matukio ya kuwashukuru walipakodi wa mkoa huo.



Katibu Tawala Mkoa wa Tanga, Pili Mnyema (kushoto), akijadili jambo na Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfakia, baada ya kumalizika mkutano wa kusikiliza kero za watumishi wa serikali wa kada mbalimbali Tarafa ya Ngomeni uliofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Utafiti wa Kilimo na Udongo cha TARI Mlingano. Kulia ni Ofisa Utumishi Mwandamizi kutoka Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa, Ramadhan Ally. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Vijana watakiwa kuchangamkia fursa ughaibuni

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Baraza la Biashara nchini Kenya, Stanley Kiplagat amewashauri vijana nchini kuacha woga wa kuchangamkia fursa za kufanya kazi katika kampuni za kigeni na nje ya nchi ili kujikwamua na umaskini.

Vilevile amewashauri waliofanikiwa kupata kazi ughaibuni kuwa mabalozi wazuri wa Tanzania na wanaporejea nyumbani baada ya mikataba yao kumalizika wajikite kwenye uwekezaji wa miradi ya kiuchumi ili kuwakwamua wenzao na umaskini.

Kiplagat alitoa ushauri huo wakati wa uzinduzi wa Kampuni ya Savanna Recruitment Business Company uliofanyika jijini hapa jana.

"Ukienda kufanya kazi huko, kesho utakuwa balozi mzuri sana kwa Watanzania wengine. Vijana msiogope kwenda ughaibuni fursa za kujikwamua kiuchumi zipo nyingi mzitumie ili mnaporudi mnawekeza nyumbani," alisema.

Alisema endapo vijana wakichangamkia fursa zilizopo nchini Romania ambako kampuni hiyo imekuwa ikiwapeleka kufanya kazi watachangia uchumi wa taifa na kujikwamua na umaskini kwenye familia zao ambazo bado ni tegemezi na kubuni biashara pindi mikataba ya kazi inapomalizika na kurudi nyumbani kuwekeza zaidi.

"Ukienda kufanya kazi huko, kesho utakuwa balozi mzuri sana kwa Watanzania wengine, vijana msiogope kwenda ughaibuni fursa za kujikwamua kiuchumi zipo nyingi, mzitumie ili mnaporudi mnawekeza nyumbani," alisisitiza.

Kabla ya uzinduzi huo, Mkurugenzi wa Kampuni hiyo Tanzania, Tudor Nistor, alisema vijana wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wakiwamo wa Tanzania, wanapaswa kutumia fursa zilizopo nchini Romania kuwekeza nchini na kuwainua wenzao kiuchumi.

Nistor, alisema vijana wa EAC wanajulikana zaidi kwa uchapakazi na ujuzi katika ufundi na ubunifu hasa katika kilimo.

Rares Simedrea, Mkurugenzi Mwenza wa Kampuni hiyo, alisema Tanzania na Romania zina uhusiano mzuri wa kidiplomasia, hivi karibu Rais wa nchi hiyo alikutana na Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kuimarisha masuala ya kiuchumi, biashara, uwekezaji, utalii na uchumi wa bluu.

Ofisa Kazi wa Mkoa wa Arusha, Flaviana Chacha, alisema nafasi hiyo ni nzuri na haijaja kwa bahati mbaya, kwa kuwa filamu ya The Royal Tour iliyozinduliwa na Rais Samia imefungua fursa za uwekaji nchini.



# Waziri Simbachawene awaonya watumishi kudharau wananchi

**Na Benny Kingson,** TABORA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amewaonya watumishi wa umma kuacha tabia za kuwadharau wananchi na kuhakikisha wanawapa huduma stahiki bila kujali hali za maisha.

Simbachawene alitoa onyo hilo juzi wakati wa mahafali ya 38 ya Chuo cha Utumishi wa Umma cha Uhazili mkoani hapa.

Simbachawene aliwataka watumishi kutambua kuwa wameajiriwa na wananchi, hivyo jukumu lao kubwa ni kuwatumikia kwa weledi na kutatua matatizo yao kwa wakati.

"Tambueni kuwa utumishi wa umma ni ibada, hivyo hakikisheni utumishi wenu unakuwa bora kupitia huduma mnazozitoa kwa utiifu, upole, uadilifu na usikivu kwa wale mnaowahudumia," alisema.

Kwa upande mwingine, aliagiza watumishi wanaoajiriwa kupatiwa mafunzo ya awali na kuwajengea umahiri kabla ya kuanza kazi ili watambue miiko na kurahisisha utoaji wa huduma katika ofisi za umma.

Simbachawene, alisema serikali inatarajia kukifanyia ukarabati chuo hicho ili kiwe katika ubora kwa sababu kinaandaa, kutoa watumishi na kufanya tafiti bora za utawala.

Awali akitoa taarifa ya utendaji kazi chuoni hapo, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Ernest Mabonesho, alisema wameongezeka watumishi 278 kutoka 242 ili kuongeza kasi ya utendaji kazi.

**"Tambueni kuwa utumishi wa umma ni ibada, hivyo hakikisheni utumishi wenu unakuwa bora kupitia huduma mnazozitoa kwa utiifu, upole, uadilifu na usikivu kwa wale mnaowahudumia," alisema.**

"Tuna upungufu wa kompyuta, vifaa vya uchapaji, miundombinu, majengo ni ya zamani tangu mwaka 1972 chuo kinaanzishwa, madarasa hayakidhi mahitaji pamoja na gharama za uendeshaji kuwa kubwa," alisema na kuongeza kuwa: "Pia tutajitahidi kujenga majengo ya chuo katika mikoa ya Singida, Tanga na Mbeya ili kuacha kuendelea kupanga."

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batrida Burian kwenye mahafali hayo, Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Louis Bura, aliwasihi wahitimu hao kuendeleza weledi waliopata chuoni hapo watakapokuwa ili kuisaidia jamii na Taifa.




Mratibu wa Taasisi ya Waandishi wa Habari ya InfoNile nchini Tanzania, Said Sindo, akitoa maelekezo kwa waandishi wa habari kuhusu jukwaa la NileWell linalowaunganisha waandishi wa habari na wataalamu wa utafiti mbalimbali wa kimazingira ili kupata kwa urahisi na haraka kurahisisha shughuli za uandishi. Jukwaa hilo lilitambulishwa kwa mara ya kwanza nchini juzi jijini Mwanza. **PICHA:VITUS AUDAX**

## Mbunge awapasha wazazi hakuna ajira serikalini

**Na Alex Sayi,** MASWA

MBUNGE wa Jimbo la Maswa Magharibi mkoani Simiyu, Mashimba Ndaki amewataka wazazi kuwasomesha watoto wao wahitimu wa vyuo vikuu nchini fani za ufundi ili kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira nchini.

Ndaki alitoa rai hiyo juzi katika mahafali ya 47 ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Malampaka wilayani hapa.

Alisema wazazi wanatakiwa kuangalia fursa za kusoma kwenye vyuo vya ufundi ili waweze kujiajiri badala ya kusubira ajira serikalini ambazo kwa sasa hakuna.

"Nitatoa mfano mzuri kwa watoto wangu licha ya kumaliza vyuo vikuu hakuna aliyeajiriwa mbali na mimi kuwa na uwezo wa kuongea uso kwa uso na waziri mwenye dhamana. Wazazi somesheni watoto mkijua ajira kwa sasa hakuna serikalini changamkieni fursa za ufundi wajiajiri," alisema Ndaki.

Mhitimu wa chuo hicho, Josephina Lucas, alisema kati ya wanafunzi walioanza masomo ya ufundi chuoni hapo 135 ni 124 wamehitimu.

Rais wa Wanafunzi wa chuo hicho, Charles Joseph, alisema elimu aliyopata na wahitimu wenzake, itawasaidia kuingia moja kwa moja kwenye soko la ajira kwa kujiajiri wenyewe.

Akitoa taarifa ya chuo hicho, Mwalimu Noel Shigolo, alisema kilianza kutoa mafunzo mwaka 1978 kwa lengo la kuwawezesha vijana kupata elimu ili kuondokana na adui umaskini, ujinga na maradhi.

Mkuu wa chuo hicho, Michael Mahundi, alisema serikali imetoa mashine za kisasa, vifaa vya kufundishia na kujifunzia vyenye thamani ya Sh. milioni 208 za Covid 19.

Mahundi, alisema serikali imetoa zaidi ya Shilingi milioni 300 kwa ukarabati, ujenzi wa jengo la utawala, madarasa, vyoo na mabweni.

**Rais wa Wanafunzi wa chuo hicho, Charles Joseph, alisema elimu aliyopata na wahitimu wenzake, itawasaidia kuingia moja kwa moja kwenye soko la ajira kwa kujiajiri wenyewe.**

# Mtanda awafunda wafanyabiashara fursa za mgodi

**Na Timothy Itembe,** MARA

WAFANYABIASHARA mkoani hapa wametakiwa kutumia fursa ya Mgodi wa Barrick kuleta maendeleo na kuongeza ajira kwa vijana.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, wakati akifungua mafunzo ya wafanyabiashara yaliyoandaliwa na Kampuni ya Mgodi wa Barrick North Mara kwa ushirikiano na Kampuni ya Impacten Africa.

Mtanda, alisema kupitia mgodi huo kuna fursa za biashara ambazo zitawasaidia wafanyabiashara hayo kuinua mitaji yao na kuongeza mzunguko wa fedha za ndani na za kigeni mkoani hapa.



Aliwataka vijana mkoani hapa kuacha tabia za kuvamia mgodi huo kwa lengo la kuiba mchanga unaodhaniwa kuwa na dhahabu kwani kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

Alisema badala ya kujihusisha na vitendo hivyo, vijana hao wanatakiwa waunde vikundi vya kijamii vinavyotambulika kisheria ili wawezeshwe kwa kupatiwa mitaji ya kuanzisha miradi ya ujasiriamali na kujiingizia kipato.

"Mgodi huu umekuwa na tija kwa taifa ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wafanyabiashara, vijana na shughuli mbalimbali za serikali ikiwa ni pamoja na kutoa zaidi ya Shilingi bilioni 70 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya shule, hivyo tuwape ushirikiano katika shughuli za maendeleo, " alisema Mtanda.

Kaimu Meneja wa Mgodi wa Barrick North Mara, Hermence Lulah, aliwataka wanufaika wa mafunzo hayo kuwa mabalozi kwa kueleza manufaa ya mgodi huo kwa taifa na jamii.

" Sheria inatutaka kuwajengea uwezo wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli zetu na mzunguko wa uchumi wa uchimbaji madini, " alisema Lulah.

Mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo, Bhoke Johnbosco, alisema kuna haja serikali kushirikiana na mgodi kuona namna ya kuwatengea vijana maeneo ya kuchimba madini ya dhahabu katika migodi iliyopo mkoani Mara li kuondokana na tamaa ya kuvamia mgodi huo.



Ukurasa 12

Shujaa kutoka kibanda cha tembe hadi kumiliki hekalu



Ukurasa 13

Makarani wanavyowatonesha vidonda wanawake wanaodai matunzo ya watoto

Nipashe

TESA

Jumanne Novemba 28, 2023

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

Vipengele sheria ya mtoto, TAKUKURU vibadilike, kukomesha rushwa ya ngono

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

## MIAKA 36 TAMWA TAMU

# Ni jicho angavu, mtetezi wa wote yatamani Tanzania bora kwa wote

MWAKA 1987, Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), kinaundwa na mwaka huu kimetimiza miaka 36 ya harakati.

Ili kuangalia nyuma na kutafakari mafanikio ya juhudi za wanawake kujikomboa na kujiletea maendeleo, leo na kesho WANATAMWA pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan, wanajumuika pamoja jijini Dar es Salaam, kutafakari safari.

TAMWA inayofananishwa na jicho pevu linaloona kila kona hadi mafichoni likitaka usawa wa kijinsia, fursa na haki sawa kwa wote,inafanya kampeni zake kupitia vyombo vya habari .

Inaamini kuwa runinga, mitandao ya kijamii, magazeti, redio na ruinga za mitandaoni ni baadhi ya njia za kufikisha ujumbe wa habari na kuleta mabadiliko.

Kwa miaka 36, ikiongozwa na Wakurugenzi ambao ni wanahabari nguli Fatma Alloo, Leila Sheikh, Dk. Ananilea Nkya, Vallerie Musoka, Edda Sanga na sasa Dk. Rose Reuben, ina mengi ya kujivunia.

Mojawapo ililoafanyia kazi ni ujio wa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA), iliyoharamisha udhalalishaji udhalilisha kingono na ukeketaji.

Aidha, ina jina kubwa Bara na Visiwani kote ikiwa na ofisi za kisasa. Tena inajivunia kusomesha wanachama wake ambao wamefikia hata ngazi za shahada za ubobezi kwa kutumia mbinu na rasimali zake.



Mkurugenzi Mtendaji TAMWA, Dk. Rose Reuben. **PICHA: SABATO KASIKA**

Jambo mojawapo inalilipigania hata leo taifa kuwa na sheria bora za barabarani, kwa kuguswa kuwa ajali zinamaliza Watanzania kila mahali na kila wakati na kupaza sana sauti kubadilisha sheria ya usalama barabarani kulinda uhai.

Hebu fikiria abiria 60 wanapopata ajali na wengi wakafariki, ni sawa kusema nchi imefiwa, kwa vile ajali imeondoa nguvu kazi ya aina mbalimbali inayopotea kwa muda mfupi.

Ajali zimeua mamilioni, kuongeza wanaoishi na ulemavu, wagonjwa wa maisha, wategemezi wagane, wajane, yatima na kuangamiza nguvukazi ya taifa kwa kasi. Ni jambo mtetezi na sauti ya Mtanzania hakulinyamazia.

TAMWA inaiomba serikali ifanye jambo, ikizifananisha ajali na moto unaoteketeza watu na mali bila huruma, lakini ungezuilika kama jiko la mkaa lisiwekwa chini ya pazia dirishani.

TAMWA inakumbusha kurekebisha Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973 ili kupunguza ajali zinazoua,kujeruhi na kuongeza umaskini wa familia na taifa linaloachwa wategemezi, walemavu wa kudumu na yatima.

Aidha taifa likitumia mabilioni ya bajeti ya afya kutibu majeruhi, lakini vyote vikiongeza mzigo kwa mwanamke anayetunza familia, kulea wagonjwa na kubakia mjane

Kuanzia 2015 hadi 2021 TAMWA inamsemea Mtanzania asifie barabarani kwa sababu sheria yake ya usalama siyo madhubuti kumbana dereva au abiria asiyejali maisha.

Inafanya kampeni kupata sheria inayomlazimisha kila msafiri kuvaa mkanda muda wote akiwa safarini. Ni upungufu, sheria haitamki kuwa kila mmoja avae mkanda licha ya kwamba magari yote yana mikanda.

Sauti ya abiria TAMWA inataka sheria kutamka ulazima wa kuvaa mkanda baada ya kugundua kuwa, hata magari ya masafa au ya mikoani hakuna sheria ya kuvaa mikanda ya usalama.

Ndiyo, abiria wanavaa lakini ni kanuni zilizotengenezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafirishaji Ardhini na Majini (SUMATRA) wakati huo na sasa na LATRA ikisimamia usafiri ardhini.

Kadhalika ndizo zilizowalazimisha madereva wa daladala mijini kuvaa mikanda na pia abiria aliyekaa kushoto kwao na hilo ndilo linaloendelea mpaka sasa.

Si daladala, gari binafsi, ya serikali au basi la masafa abiria wake kubanwa kisheria kuvaa 'siti belti' yote hayo yakichochea ajali

Aidha, TAMWA, inawasemea watoto, kwa kushauri sheria iweke kipengele cha kuwapo viti vya watoto vyenye mikanda yao maalumu.

Ni badala ya kuwasimamisha karibu na dereva kwa upande wa daladala na hata kwenye magari binafsi kuwaacha kukalia viti vya wakubwa na kuhatarisha maisha ajali ikitokea.

Inapendekeza viti kwa watoto wenye miaka mitano kwa ajili ya ulinzi na usalama wa wasafiri hawa wadogo.

**KOFIA ZA BODA**

Zama hizi boda imekuwa kitanzi maana mamia wamepoteza maisha Bara na Zanzibar, mtetezi wao inapaza sauti kuwa uvaaji wa kofia ngumu uwe sheria kwa wote.

**INAENDELEA UK.12**

## SIKU 16 KUPINGA UKATILI

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Shujaa kutoka kibanda cha tembe hadi kumiliki hekalu

WAKATI wanawake kwa pamoja kote duniani wanaendeleza harakati za kukomesha ukatili wa kijinsia ndani ya Siku 16 za Kupinga Ukatili mwanamama Yustina Lucas, ana jambo lake. Ni kutangaza mafanikio ya mwanamke.

Ni mkazi wa Kijiji cha Wishiteleja, wilayani Kishapu mkoa wa Shinyanga, anayethibitisha kuwa mwanamke anaweza na kupitia kilimo cha umwagiliaji wa matone, ameondokana na maisha duni ya kuishi ndani ya kibanda cha tembe na sasa anamiliki nyumba ya kisasa.

Ikumbukwe tembe, nyumba inayojengwa kwa mchanganyiko wa kinyesi cha ng'ombe na udongo na kuezekwa kwa nyasi ni mara nyingi ni makazi ya watu wenye kipato kidogo.



Yustina Lucas, akifurahia nyumba yake ya kisasa, aliyojenga kupitia kilimo cha mboga kwa umwagiliaji. **PICHA: MARCO MADUHU**

Akiwa na familia ya watoto watano, ametoka kimafanikio na kinachomtoa ni kutumia mafunzo ya kilimo cha mboga anazozimwagilia kwa matone akisema kimemuondoa kwenye umaskini na sasa anamiliki nyumba ya kisasa na anamudu maisha yake.

Anatoa simulizi hiyo wiki iliyopita kwa viongozi wa wilaya ya Kishapu wakiwamo, Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, maofisa kilimo, mifugo na umwagiliaji wanaowatembelea wanavijiji wakulima wa kilimo cha umwagiliaji wanaowezeshwa na Shirika la Tanganyika Christian Refugee Service (TCRS), kuona mafanikio.

Yustina anasema mwaka 2021 alijiunga na kikundi cha Shirikisho cha wakulima wa mboga wanaolima nyanya , kilichokuwa na wanachama 20 ambao wamekuwa wakipewa mafunzo na shirika la TCRS na kuwezeshwa vifaa vya umwagiliaji.

Leo ni katibu wa kikundi, anayesema wakati wanagawana mapato ya nyanya Shilingi 100,000 kwa kila mmoja, alikuwa akiweka fedha hizo kidogo kidogo na baadaye kujiunga kwenye chama cha hisa pamoja na kuanzisha ufugaji wa kuku chotara ili kuongeza kipato.

Anasema kipato kiliongezeka na akaanza kujenga nyumba imara ya matofali na bati akiachana na kibanda duni cha tembe.

Anasimulia kuwa nyumba yake ina vyumba sita na anaendelea kuijenga na ni zao la kilimo cha umwagiliaji ambacho kimemtoa kimaisha kwa vile alikuwa na hali mbaya, lakini leo maisha ni mazuri.

Mwanakikundi mwingine William Ndindi, anasema kilimo hicho kimemtoa kimaisha na amenunua kiwanja, na hivi karibuni ataanza ujenzi wa nyumba na kuachana na tembe. Ofisa Umwagiliaji Halmashauri ya Kishapu, Mwinula Mtwangi, anasema kilimo cha uhakika kwa sasa ni cha umwagiliaji, sababu mkulima anakuwa na uhakika wa kuvuna mazao yake.

Anasema wilaya ya Kishapu ni kame, lakini wanaweza kutumia mito michache iliyopo kwa ajili ya kufanya kilimo cha umwagiliaji, pamoja na kuendelea kuchimba mabwawa sababu wilaya hiyo kwa sasa wana mtambo wa kuchimba mifereji na mabwawa ya kilimo na kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua.

"Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kilimo cha uhakika pekee kilichobaki ni cha umwagiliaji tu masuala ya kuangalia wingu la mvua yameshapitwa na wakati," anasema Mwinula.

Ofisa Kilimo halmashauri ya wilaya Richard Mangua, anasema elimu hiyo ya kilimo cha umwagiliaji wataendelea kuitoa kwa kushirikiana na wadau hao TCRS na kuitoa katika maeneo mbalimbali kwa wananchi hasa wale ambao wapo kwenye mabonde ya maji na mabwawa.

"Nilifarijika kuona wananchi wakitumia mabonde ya maji na mito kufanya kilimo cha umwagiliaji ambacho kimekuwa mkombozi kwao, naomba tu maofisa kilimo wa kata muwatembelee mara kwa mara na kuwapatia elimu pia ya kutumia mbegu na dawa na viuatilifu kuua wadudu, ili wapate mavuno mengi,"anasema Mangua.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Kishapu, Joseph Swalala, anampongeza Yustina Lucas kwa kujiunga na kikundi cha Shirikisho kulima mboga kupitia umwagiliaji, na kutumia vyema fursa na hata kufikia hatua ya kujenga nyumba ya kisasa.

Anasema mwanamama huyo ni mfano wa kuigwa kwa sababu amekuwa akizitumia fedha vizuri ambazo hugawana kwenye vikundi na kuwekeza kwenye maendeleo.

"Vikundi hivi vya kilimo cha mboga kwa umwagiliaji vimenikosha sana na tukiruhusiwa kuanza kutoa mikopo tena nitazungumza na mkurugenzi tuone namna ya kuwapatia mikopo ya trekta ili muongeze wigo mpana wa mashamba," anasema Swalala.

Kiongozi wa mradi wa Shirika la Tanganyika Christian Refugee Service TCRS wanaotoa elimu hiyo ya kilimo cha umwagiliaji kwa wananchi kupitia vikundi kwa kushirikiana na wataalamu wa serikali wakiwamo maofisa, kilimo, mifugo na umwagiliaji, Dk. Oscar Rutenge anasema mwanamke huyo amekuwa kiongozi bora kwa kuonyesha wenzake njia ya mafanikio.

# Ni jicho angavu, mtetezi wa wote yatamani Tanzania bora kwa wote

**INATOKA UK.11**

Sheria ya usalama inaelekeza kinga hiyo dhidi ya ajali ivaliwe na dereva pekee, TAMWA ikihoji vipi, abiria ambaye naye anaweza kupondwa kichwa na kuuliwa mbona kasaulika?

Inapendekeza kofi kwa wote wa abiria na madereva, japo watu wanaona abiria wa pikipiki wanavaa kofia, ikumbukwe siyo sheria ni maelekezo ambayo mara nyingi hupuuzwa.

Wapo wanaoikataa wakiionea kinyaa na kuhisi 'helmeti' hi chafu, inaweza kuwapa mapunye, inanuka lakini wengine wakidai inawavurugia mitindo ya nywele.

TAMWA inaona kuwa kukosekana kipengele hicho kisheria kutaka uvaaji, wasafiri wanapuuza, wanapanda bodaboda tena zinazokimbia kwenye barabara kuu bila kofia kichwani na ajali zinaendelea zikileta vifo na ulemavu wa aina mbalimbali.

Aidha, kiona mbali TAMWA kinawatetea watoto kuwa wasipandishwe bodaboda kwani ni hatari kwani hawana helmeti wala hawawezi kumshikilia dereva kwa vile mikono yao ni midogo .

Ombi la TAMWA kwa serikali chonde chonde watoto wasipandishwe bodaboda badala yake waendeshe baiskeli zao lakini pia wawe na helmeti za watoto, tena si kwenye maeneo hatarishi.

Yote haya yaingizwe kwenye sheria ya usalama barabarani iliyoboreshwa.

### VIFAA KIELEKTRONIKI

Mtetezi wa wanyonge katika jitihada za kutaka msafiri awe salama anatafakari haya, hivi dereva mwenye abiria 60, akapigiwa simu akiuulizwa uko wapi? Kimbia nyumba yako inateketea wasafiri hao watakuwa salama?

Lakini kibaya, zaidi iwapo atapokea akiwa safarini kulekea mkoani akiambiwa mwanae kafariki kwenye ajali baada ya bodaboda aliyopanda kugongwa na basi la mwendokasi jijini Dar es Salaam itakuwaje?

Ikumbukwe anayempigia simu ni msamaria aliyeona namba ya mzazi kwenye daftari la mtoto wake bila kujua kuwa ni dereva wa masafa nini kitafuata?

Ukitafakari na TAMWA ni wazi usalama wa abiria hao utakuwa shakani hivyo ujio wa sheria inayokataza simu barabarani haukwepeki, itamke hairuhusiwi kuendesha huku ukiongea au kuchati, dereva anapokuwa kwenye usukani asiguse simu na itoe adhabu kali.

Ndicho TAMWA inachokidai kwa kikosi cha usalama barabarani, Wizara ya Mambo ya Ndani, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Katiba na Sheria pia kwa wabunge.

TAMWA wakati inasherehekea miaka 36 ya kazi za uchechemuzi, (advocacy) inaishukuru serikali kwa kuiangalia sheria hiyo yenye miaka 50 ambayo mwaka jana Februari iliifikishwa bungeni na kusomwa kwa mara ya kwanza.

Baada ya mchakato imerudi kwenye kamati lakini leo ni 2023 ajali zinaua hospitali zinatibu,kukata viungo na familia zinaendelea kutunza walemavu, kubaki na uchungu wa vvifo vya wapendwa wao.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Makarani wanavyowatonesha vidonda kinamama mahakamani


Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akiwa na watoto wa Kijiji cha Nyamanzi, Mkoa wa Mjini Mgharibi, Unguja. **PICHA: IKULU**

Ni jambo la kutafakarisha ndoa nyingi zinapozovunjika, mateso yanawageukia wanawake na watoto, licha ya wazazi wa kiume kunyooshewa kidole kukwepa wajibu wa kuhudumia familia.

Talaka inapotolewa kuvunja ndoa inageuka adhabu kwa mama lakini na watoto wasio na hatia huiteseka kutokana na wazazi kusambaratika.

Hukumbwa na njaa vijijini,hukosa mahitaji muhimu ya shule kama sare, vitabu na daftari, tiba huwa changamoto na kubwa zaidi hukwama kutimiza azma au ndoto za maisha yao.

Mzigo wa matunzo ya watoto baada ndoa 'kufa'unamlazimisha mama kuhangaikia watoto kuwapa mahitaji hasa chakula, matibabu vifaa vya elimu na makazi.

Ndiyo msemo ng'ombe hashindwi na nundu yake, ambao kinamama huutumia visiwani Zanzibar katika kupigania ustawi wa watoto licha ya kutelekezwa, kutalikiwa na kuachiwa mzigo baada ya ndoa kusambaratika.

Wapo wanaovifikia vyombo vya sheria kudai matunzo ya mtoto kutoka kwa baba zao na wengi ni wale wenye kipato kidogo hivyo hukimbilia mahakama kufungua kesi.

Hatua ya kufungua kesi mahakamani imekuwa ikilalamikiwa na baadhi ya wanawake kwa sababu ina gharama za hati za madai mahakamani lakini mawakili nao wanadai chao.

"Unapofungua kesi ya matunzo, fedha zinahitajika, fomu ya hati ya madai unaipata kwa Shilingi 10,000 bado gharama za mawakili zinakusubiri, "anasema Asha Khamis (40), ambaye alitelekezwa na watoto watano.

Anasema alilazimika kushitaki kumfungulia mume mashtaka ya madai ya matunzo ya watoto, mzazi mwenzake aliyemtelekeza zaidi ya miaka mitatu sasa.

Anasema watoto wote bado wanahitaji kupata elimu anayoigharamia peke yake, akisema ni mzigo mzito kwake akihoji kwanini mume ashindwe kutoa matunzo wakati anafanya kazi ambayo inamuingizia kipato?

Aidha, amefungua hati ya madai ya matunzo wa watoto inayohitaji gharama, lakini alipambana kumudu gharama hiyo na kuruka kiunzi iliamuriwa baba watoto kutoa matunzo ya watoto kila mwezi.

Asha ameonyesha ujasiri wa kufika mahakamani kudai matunzo ya watoto, jambo ambalo wanawake wengi hawana ujasiri huo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukosa uelewa wa masuala ya kisheria, linampa ushindi zaidi.

Mwanakheri Khamis (35) mama wa watoto watatu, anasema wanawake waliotelekezwa na watoto wanahitaji kupatiwa msaada kisheria ili kuwa na ujasiri wa kudai haki zao yakiwamo matunzo ya watoto.

Anashauri elimu iende sambamba na kuondoa gharama za hati za madai mahakamani hasa kwa kesi za talaka na madai ya matunzo ya watoto.

"Ukiona mwanamke amekwenda mahakamani kudai talaka au matunzo ya watoto ujue maji yameshamfika shingoni, wengi wanapitia mateso na manyanyaso mengi kwenye ndoa zao," anaeleza.

Ofisa msimamizi kitengo cha kupinga ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kutoka Chama Cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar), Zaina Salum Abdallah, anasema kesi nyinyi za matunzo ya watoto zinapelekwa mahakamani, sehemu ambayo hakuna huduma ya msaada wakisheria.

Aidha, TAMWA inapokea malalamiko yanayohusiana na ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto kukoseshwa haki zao hasa matunzo.

Katika kukabiliana na tatizo hilo, chama kimewekeza nguvu zaidi kwa kuendelea kutoa elimu kwa jamii, kupata uelewa wa kuzitumia taasisi zinazotoa msaada wa kisheria ikiwamo kupata hati za madai ya matunzo.

Fatma Khamis Ali, msaidizi wa huduma za kisheria Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, anasema kuna madai ya makarani wa mahakama kuomba mlungula kutoka kwa wanawake wanaofika kudai matunzo.

Anasema wanapokea malalamiko kutoka kwa wanawake hao wakisema wanatozwa fedha na baadhi ya makarani mahakamani.

Wasaidizi wa sheria kazi yao kubwa ni kutoa msaada ya kisheria kwa wananchi hasa wale wanaokumbwa na udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo kutelekezwa, anasema.

Huwasadia na kuwaongoza jinsi ya kufikia vyombo vya kisheria kwa ajili ya kupata haki na wapo baadhi ya wanawake walitelekezwa na wenza wamewapeleka sehemu sahihi kushughulikia kesi ya madai na kupata haki, anaongeza.

Ofisa sheria kutoka idara ya msaada wa kisheria, Salma Suleiman, anasema idara hiyo imesaidia na kutoa ushauri wa kisheria kwa wananchi wakiwamo wahanga wa vitendo vya udhalilishaji.

Anasema miongoni mwa ushauri wanaotoa ni kuhakikisha wahanga hao wanaripoti kesi hizo polisi ili kuzifikisha mahakamani kupata haki.

> Ukiona mwanamke amekwenda mahakamani kudai talaka au matunzo ya watoto ujue maji yameshamfika shingoni, wengi wanapitia mateso na manyanyaso mengi kwenye ndoa zao.

Kadhalika huwasaidia kuandaa hati ya madai bila gharama kwani hugharamiwa na idara ya msaada wa kisheria.

Anasema idara hiyo imeshawafikia wananchi 4,339 wakiwemo wanawake 2,592 na wanaume 1,747 katika kuwapatia ushauri na msaada wa kisheria kupitia wasaidizi wa msaada wa kisheria kwa mwaka 2020/2021 ambapo kila wilaya za Unguja na Pemba inawasaidizi hao.

Hata hivyo anasema licha ya kuwa na wasaidizi wa shehia kila wilaya lakini nguvu za ziada zinahitajika kuongeza wasaidizi wa kisheria ili kila shehia kuwepo kwa wasaidizi hao hasa kwa maeneo ya pembezoni akitoa mfano Kisiwa cha Fundo Pemba.

Kadhi Dhamana Wilaya ya Mwanakwerekwe Omar Shekha Khamis, anasema wanawake wanaofika katika mahakama hiyo kwa ajili ya kudai matunzo ya watoto huwaelekeza waende Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) au, kituo cha huduma za sheria.

Akizungumzia kuhusu madai ya kesi hizo kuchelewa, anasema utaratibu unaotumika unazingatia ukubwa wa tatizo na namna ya uhudhuriaji wa wahusika wa kesi na kwa wastani husikiliza kesi nne kwa siku zinazohusu madai ya matunzo ya watoto.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Vipengele sheria ya mtoto, TAKUKURU vibadilike kukomesha rushwa ya ngono

IWAPO wewe ni dereva wa chombo chochote, unayeghilibu, kuhadaa wanafunzi na kuwanyanyasa kingono kwa minajili ya kuwazawadia usafiri, fahamu unachimba kisima, utatumbukia kwanza.

Kama ulivyo msemo mchimba kisima huingia yeye, umejichimbia kaburi, anasema Ali Mcheni dereva wa bajaji mkazi wa Dar es Salaam, anayekemea kutumia lifti kunyanyasa wanafunzi.

Ni katika mazungumzo na Nipashe, anapoeleza kuwa madereva wanawalaghai mabinti kuwapa mimba, kuwavurugia masomo, kuwaambukiza maradhi na hata kuharibu hatma zao, lakini wanachofanya kitawageukia.

"Watoto wao wanatendewa vivyo hivyo na madereva wengine kwenye maeneo wanapofanya kazi."

Mcheni, anatoa ushuhuda baada ya kujengewa ujasiri na shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), linalofunza madereva kubadilika, kuacha kuomba wanafunzi rushwa ya ngono wakiwalipa lifti.

Anaonya madereva kushiriki ngono na wanafunzi ni kuhamishia matatizo nyumbani kwao, mfano iwapo dereva atabaka wanafunzi popote alipo, kadhalika madereva wengine kwenye vituo vyao popote walipo wanafanya hayo na inawezekana yakamkumba binti yake.

"Mfano boda uko Mbezi au Kariakoo ukiomba mwanafunzi au mtoto rushwa ya ngono kwa hadaa za lifti na zawadi nyingine, ujue huko Chalinze, Tunduma au popote Tanzania wapo madereva kama wewe wanaofanya vivyo hivyo na inawezekana anayenaswa akawa binti, mpwa, mdogo wako."

Mcheni anasema baadhi ya madereva wa boda, bajaji, daladala, mabasi ya masafa wanachukulia poa huwatumia wanafunzi kingono, wakiona ni kawaida bila kujua kuwa ni tatizo linalozunguka kila mahali na kuathiri taifa kwa kuwa ni mienendo ya madereva wengi popote walipo.

"Kuna msururu wa mikasa ya kunyanyasa watoto kuanzia kisaikolojia, kimwili na linaloshika kasi zama hizi ni ngono," anasema Mcheni.

Wasichana kwa wavulana wananyanyaswa kuanzia kwenye familia, jamii inayowazunguka yenye watoa huduma muhimu vikiwamo vyombo vya usafiri, anaeleza.

Rushwa ya ngono kwa wanafunzi na watoto ni mzigo. Watoto wajitoe kwa dereva wafikishwe



Janeth Mawinza Mkurugenzi Mtendaji wa WAJIKI **PICHA: MTANDAO**

> Wasichana wanasema pale wanapokubali madereva wanaanza kuwafuatilia shuleni , mitaani na kuwapa lifti, zawadi, simu na wengine wakionyeshwa sehemu za kujibanza ili kusubiri usafiri huo.

shuleni, warudishwe nyumbani na kubebwa siku zote bila gharama. Tena wanazawadiwa simu ili kuwasiliana, anasema Janeth Mawinza, akimuunga mkono Ali Mcheni.

Janeth ni Mkurugenzi Mtendaji wa WAJIKI, inayofanya kampeni za kupambana na rushwa ya ngono kwa wanafunzi wa sekondari na msingi jijini Dar es Salaam.

Katika mazungumzo na Nipashe wakati huu wa Kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili Kijinsia, anasema wanafunzi wanalalamika rushwa hiyo imezidi.

Anaeleza kuwa walianza kampeni za kuhamasisha uelewe na kukwepa mimba za utotoni shuleni, lakini ndani ya mchakato huo wanafunzi wakawaeleza kuwa shida inayochochea mimba ni rushwa ya ngono kutoka kwa madereva.

Kwa ufadhili wa Mfuko wa Ruzuku kwa Mashirika ya Wanawake (WFT-T), kuanzia mwaka 2018, WAJIKI imetafiti na kuibua ukweli wa maelezo ya wanafunzi kwenye shule kadhaa za Dar zikiwamo za kata ya Makumbusho na Mwananyamala manispaa ya Kinondoni na kuanzisha kampeni kwa madereva kuhamasisha kuacha mienendo hiyo.

Wanaofikiwa ni madereva wa daladala, boda, bajaji, mabasi ya mijini na hata ya masafa marefu na huo, ukiwa mwanzo wa kuzifikia wilaya zote za Dar es Salaam.

Anafafanua kuwa wasichana wanaeleza udanganyifu unavyofanywa pengine kwa mtindo wa kuwahurumia au kuwasifia mfano, 'mrembo unasoma wapi, panda twende.'

Wengine huwaambia 'mrembo umependeza au mtoto unalipa' wapo baadhi husogeza boda au bajaji hata basi karibu na kuwaambia binti panda chomboni.

Aidha, madereva na makonda wa daladala wanaweza kusimamisha gari na kuwabeba lakini wakiendelea kupenyeza ujumbe wa rushwa ya ngono kimasihara na ujanja, yote hayo yanaanza na mazingira ya kuwasaidia usafiri.

"Wasichana wanasema pale wanapokubali madereva wanaanza kuwafuatilia shuleni , mitaani na kuwapa lifti, zawadi, simu na wengine wakionyeshwa sehemu za kujibanza ili kusubiri usafiri huo," anasema Janeth.

**KUGEUKIA MADEREVA**

"Madereva tunapozungumza nao wanasema uhusiano na mabinti hasa wanafunzi walionao kama sehemu ya maisha, lakini tukawaambia ni lazima kubadilika kuacha kunyanyasa watoto wenu."

"Nikawaambia inamaanisha unapobaka, kumpa mimba mwanafunzi kwenye kituo chako mfano Makumbusho au Manzese ni kama unajihamishia matatizo nyumbani. Ni kwa sababu dereva mwingine atafanya hayo hayo kwa binti yako popote alipo," anasema Janeth.

"Hapo ndipo tukaanza kampeni, tumefikia zaidi ya madereva 8,000 wa vyombo mbalimbali kuanzia boda, bajaji hadi mabasi ya masafa. Kampeni yetu "Acha badilika safari salama bila rushwa ya ngono inawezekana," anaongeza.

Mikutano ya kampeni inaendelea na imefanyika maeneo kama kituo cha Mbagala, Gongo la Mboto na Mbezi, WAJIKI ikitumia mabango, fulana, stika na vizibao (reflectors) vyenye ujumbe 'safari salama bila rushwa ya ngono inawezekana'.

"Vyote vinapeleka ujumbe na vinaamsha mijadala. Jamii, wanafunzi, kinamama wote wanaongea rushwa ya ngono. Boda na bajaji zinafika karibu kila kona zikiwa na mabango ya ujumbe, naamini umesambaa sana ndiyo maana watu wamevunja ukimya."

Anawashukuru wanaofikisha kesi WAJIKI kuomba msaada, pia kuelekezwa kwenda mahakamani, akisema ni kutokana na kampeni kuwafunza mabinti mbinu za kukataa, kujiepusha na mambo yanayowafikisha kwenye rushwa ya ngono.

Anataja, mfano kukataa kujihusisha na ngono utotoni, kuacha zawadi za wanaume, kuelezwa hatari na athari za ngono ukiwamo ujauzito na maradhi, kuachishwa shule, kuwajulisha sehemu za kutoa taarifa na watu wanaotakiwa kuwaambia, kuwaeleza sheria zinazowalinda na kuwaadhibu wanaowaomba rushwa ya ngono.

Aidha, madereva kufahamishwa, athari, sheria zinazowabana mfano ya Mtoto, ya Makosa ya Kujamiiana na ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

**WANACHOLENGA**

Edward (la pili linahifadhiwa) ni mwanafunzi wa kidato cha pili, Sekondari ya Urafiki iliyoko Ubungo jijini, anayesema serikali iwasaidie wanafunzi kupata usafiri na mabweni kuwaepusha na ulaghai wa madereva.

"Mimi na wenzangu tunasoma Urafiki tunasimama kituoni Manzese kusubiri magari ya mwendokasi kuanzia saa 11 hadi saa 1 jioni, kila likipita limejaa hakuna nafasi. Hatuwezi kupanda. Daladala, bajaji zinakataa nauli ya 200.Tunafanya nini? Anahoji.

Anashauri serikali iwekeze kwenye usafiri kwa kuwa hakuna amani kwa mwanafunzi kama kila siku anawaza anafika shuleni na kurudi nyumbani kwa kukosa usafiri.

Anaamini inawezekana taifa likiamua. Rushwa ya ngono na madereva au yeyote itapungua au kuisha iwapo kuna usafiri salama kwa wanafunzi wote.



## Wanafunzi 8,000 afya na sayansi wakopeshwa mabilioni

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imetenga Shilingi bilioni 48 kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi 8,000 wa ngazi ya stashahada katika fani za afya na sayansi shirikishi kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Jenifa Omolo, aliyasema hayo kwenye mahafali ya 37 ya Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP) yaliyofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita jijini hapa.

Omolo alisema serikali imetoa kiasi hicho kwa mwaka huu wa fedha wa 2023/24 kwa sababu imedhamiria kuongeza wataalamu wa masomo hayo ili kutekeleza maazimio ya Afrika kuhusu rasilimali watu.

Fani nyingine ni elimu, masomo ya fizikia, hisabati, kemia, amali usafiri na usafirishaji, uhandisi wa nishati, madini, sayansi ya ardhi, kilimo na mifugo.

Aliendelea kusema kuwa serikali itaendelea kuongeza bajeti ya mikopo ya elimu ya juu kwa lengo la kuwawezesha vijana wengi kunufaika.

Alifafanua kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2023/24, Shilingi bilioni 731 zimeongezeka ikilinganishwa na Shilingi bilioni 570 zilizotengwa 2022/23 kwa ajili ya kukopesha wanafunzi waliojiunga na vyuo vikuu.

"Hii ni ongezeko la asilimia 28. Wanufaika wameendelea kuongezeka kila mwaka, mwaka jana walikuwa 177,777 na mwaka huu ni 220,376 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 23," alisema.

Alisema serikali kupitia Samia Scholarship imeongeza kifurushi kingine cha mkopo wa elimu ya juu ili kuwahamasisha watoto wa kike kusoma masomo ya sayansi na watakaofanya vizuri watapewa mkopo wa asilimia 100.

"Ili wasome kozi za fani za teknolojia, uhandisi hisabati na tiba (STEM) Serikali kwa mwaka wa masomo 2023/24 imetenga jumla ya shilingi bilioni 6.7 na programu hii ilianza mwaka jana 2022/23 lengo ni kuongeza wataalamu wa kike katika fani hizo zilizotaja hapo juu," alisema na kuongeza kuwa:

"Mbali ya kuongezeka kwa bajeti ya mkopo wa elimu ya juu kila mwaka, katika mwaka huu wa masomo 2023/2024, serikali yetu chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imeweza kutenga fedha hizo kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi hao wapatao 8,000," alisema.

Mkuu wa chuo hicho, Profesa Hozen Mayaya, alisema katika mwaka wa fedha wa 2022/23 chuo hicho kiliendesha mafunzo ya muda mrefu katika programu 26 katika fani mbalimbali.

Profesa Mayaya alisema programu hizo ni kuanzia ngazi ya astashahada hadi shahada za uzamili.

Alizitaja fani hizo ni mipango na maendeleo, mipango utawala na usimamizi wa maendeleo, uchumi wa maendeleo, mipango na usimamizi wa miradi mipango usimamizi wa mazingira maendeleo ya miji na usimamizi wa mazingira idadi ya watu na mipango ya maendeleo.

Nyingine ni maendeleo ya jamii, mipango ya fedha za maendeleo na uwekezaji, Mipango na usimamizi wa rasilimali watu mipango na usimamizi wa biashara pamoja na utawala na maendeleo endelevu.

# Wizara yalia uhaba wahandisi wa vifaa tiba hospitali nchini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TANZANIA inakabiliwa na uhaba wa zaidi ya wahandisi 9,000 wa ufundi wa vifaa tiba wa kuendesha mashine za matibabu zilizopo katika hospitali za serikali nchini.

Akizungumza baada ya ufunguzi wa mafunzo ya wahandisi wa ufundi wa vifaa tiba yanayotolewa na Shirika la Afya la Kimataifa la Korea (KOFIH), Mkuu wa Huduma za Ufundi wa Vifaa Tiba wa Wizara ya Afya, Mhandisi Suniva Haule, alisema wataalamu hao wanahitajika katika hospitali za mikoa, kanda na kibingwa.

Mhandishi Haule alisema kuwa Tanzania ina wataalamu 359 katika hospitali hizo, hivyo inahitaji wataalamu hao 9,000 ili kwenda sambamba na ongezeko la mashine hizo zilizopo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa.

Kwa mujibu wa Haule, kila halmashauri ina mtaalamu mmoja na serikali inatenga bajeti ya kuajiri wataalamu hao ili kukidhi mahitaji kwenye hospitali hizo.

Alisema mwaka jana, Serikali iliajiri wataalamu 147 na kwa mwaka huu walioajiriwa ni 100. Wataalamu waliopo nchini ni 359.

Profesa Ik Keun Kim wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Kampasi ya Mloganzila, alisema matumizi ya teknolojia yameibadilisha dunia na kuwataka wanaopata mafunzo hayo kuwa chachu ya mabadiliko katika sehemu zao za kazi.

Mratibu Mkazi wa KOFIH, Gloria Kim, alisema uhandisi wa matibabu una jukumu muhimu katika utoaji wa huduma bora kutoka utambuzi hadi matibabu kwa mgonjwa.

"Kulingana na hilo, KOFIH imeanzisha mafunzo ya CEOMETS tangu mwaka 2015 ili kuimarisha uwezo wa wahandisi wa ndani na imefanikiwa kuchangia mafunzo kwa wakufunzi 216 na mafunzo ya mwaka huu yataongeza hadi wakufunzi 249," alisema.

Alisema wahandisi wa matibabu wana jukumu la kuimarisha mfumo wa afya wa kitaifa, huduma ya afya ya msingi na kufikia chanjo ya afya kwa wote.

"Kuna haja ya dharura ya mipango ya kitaifa ya kimkakati, miongozo na mipango ya nguvu kazi inayoakisi wahandisi wa matibabu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema.

Aliongeza kuwa KOFIH imefadhili mafunzo tangu 2015 kwa kuwekeza dola za Marekani 790,000 na kwamba kwa mwaka huu zaidi takribani dola 150,000.

Mhandisi Valentino Mvanga wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, alisema wataalamu wa fani hiyo wamekuwa wakiongezeka kila mwaka.

Alisema kwa sasa mashine na vifaa vingi vinatengenezwa na wataalamu wa ndani na inapotokea mahitaji zaidi wataalamu kutoka nje ya nchi wanafika na kufanya kazi hiyo..



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Kusundwa Wamalwa, akimkabidhi kadi za kielektroniki Katibu wa chama hicho, Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara, Tipis Masiaya, kwa ajili ya wanachama wake baada ya kujisajili kwa mfumo wa kielektroniki. **PICHA: PAUL MABEJA**

## COTUL yaiangukia serikali machapisho ya kielektroniki

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKISHO la Maktaba za Vyuo Vikuu na Taasisi za Utafiti Tanzania (COTUL) limeiomba serikali kulisaidia kununua machapisho ya kielektroniki kwa ajili ya kufundishia vyuoni kutokana na kushindwa kumudu gharama za ununuzi kwa bei kubwa.

Ombi hilo limetolewa na Mwenyekiti wa Shirikisho hilo, Dk. Sydney Msonde wakati wa ufunguzi wa kongamano la kisayansi la wakutubi, walimu wa vyuo vikuu nchini, watafiti na wataalamu wa Teknolojia ya Mawasiliano (IT).

Msonde alisema pamoja na kwamba lengo la COTUL ni kuhakikisha machapisho ya kielektroniki yanapatikana kwa walimu na wanafunzi ili waweze kufanya shughuli zao za msingi za kujifunza, kufundisha na kufanya utafiti nchini ununuzi imekuwa changamoto kwao kutokana na kuuzwa bei ghali.

Dk. Msonde alitoa mfano wa uchapishaji wa kanzi data inayoitwa 'Sience Direct' alisema si rahisi kwa taasisi mmoja kununua kwa sababu inauzwa dola 250,000 za Marekani.

"COTUL kazi yetu kubwa ni kuhamasisha na kuzileta pamoja taasisi zote za umma na za watu binafsi ili ziweze kuchangia kwa sehemu rasilimali fedha zitakazowezesha kununua machapisho hayo ya msingi katika kukidhi haja ya kufanya ufundishaji na utafiti nchini," alisema Dk. Msonde.

Alisema ulishaji na upatikanaji wa machapisho hayo unaweza usiwe na tija kama walimu na wanafunzi watakaokuwa wanayatumia hawatajengewa uwezo bora wa kuyatumia jambo ambalo ndilo la msingi.

Alisema lengo la kongamano hilo lilikuwa ni kujadili mustakabali wa fani ya ukutubi na namna walimu katika taasisi za umma na za binafsi wanaweza kutumia machapisho ya kielektroniki kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi nchini.

Mkurugenzi wa Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini Ofisi ya Waziri Mkuu, Sakina Mwinyimkuu, alisema shirikisho hilo limekuwa msaada mkubwa kwa serikali kwa kuisaidia kupata taarifa na maarifa ambayo kwa njia ya kawaida ingekuwa ni gharama kubwa kuyapata.

"Uwepo wa COTUL ni fursa hata kwa sisi tunaohusika na kufanya tathmini mbalimbali zikiwamo za utafiti hakika ni jukwaa muhimu sana," alisema Mwinyimkuu.

Mwinyimkuu alisema serikali itaendelea kuunga mkono kazi zinazofanywa na COTUL na kuliomba shirikisho hilo kukutana na wadau wa elimu kuona namna ya kushirikiana nao kwa kuwa kazi zao zinazihitaji na hazikwepeki hasa katika kipindi hiki ambacho dunia inahitaji teknolojia kwa ajili ya kukuza uchumi.

Mkurugenzi wa Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB), Dk. Mboni Ruzegea, alisema serikali inafanya maboresho makubwa ya maktaba kutoka katika mfumo wa kuhifadhi vitabu na machapisho mengine kwa njia ya karatasi na kwenda kwenye mfumo wa kidijitali.

Mmoja wa wafadhili wa kongamano hilo, Mkurugenzi wa Kampuni ya Totoo Ltd yenye makao yake makuu mkoani Kilimanjaro, Dk. Elvis Silayo, alisema changamoto kubwa inayowafanya watu wengi washindwe kutumia maktaba hawajui taarifa ambazo wanaweza kuzipata.

Alisema watu wengi hawapendi kusoma mambo ya taaluma, lakini maktaba kuna taarifa nyingi za kuwasaidia kupata maarifa katika maisha yao ya kila siku.

Alisema maktaba za sasa zina vitabu vilivyochapishwa kwenye miaka ya 1970 na 1980, hivyo taarifa zake haziwezi kuwa na msaada kwa mtu anayehitaji kufanya chochote kwa kipindi hiki.

Mhadhiri wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Dk. Valeria Kyumana, alisema mafunzo hayo yamewajenga kwa sababu kwa sasa teknolojia inakuwa na maktaba na huduma wanazotoa haziwezi kuendelea kwa kutumia mfumo wa zamani.





# Watumishi wanne hospitali ya rufani wasimamishwa kazi wizi wa runinga

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

SERIKALI mkoani hapa imeagiza kusimamishwa kazi kwa watuhumishi wa Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Manunuzi na Katibu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Njombe kupisha uchunguzi wa tuhuma za wizi wa runinga 15 za hospitali na kompyuta tatu.

Agizo hilo limetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, baada ya Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa kufanya kikao na watumishi wa hospitali hiyo kufuatia taarifa kuhusiana na wizi wa runinga hizo zenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni 11 na kompyuta hizo.

Mtaka ametoa siku saba kwa vyombo vya ulinzi na usalama kukamilisha uchunguzi wa tuhuma hizo ili hatua kali zichukuliwe dhidi ya watakaobainika kuhusiana na wizi huo.

"Kwanza idara ya manunuzi isimame wasije hapa ofisini kuanzia kesho, katibu wetu wa afya kwenye hospitali ya rufani asimame, asije hapa ofisini kuanzia kesho na idara ya TEHAMA," alisema Mtaka.

Alisema wizi huo umehusisha watumishi wa serikali kwa sababu hakuna mlango uliyovunjwa.

"Una dhamana, umepewa mkuu wa idara ya manunuzi, katibu wa afya una funguo ya ofisini kwako mnakubaliana watu wanne kwenye ofisi mnafungua kontena mnachukua vitu mnakwenda kuuza halafu mnatafuta namna ya kubadili kupitia ofisi hiyo hiyo hela za serikali zifanye kurejesha," alisema.

"Hali hiyo inafedhehesha utumishi wa umma kwa hiyo ni jambo la aibu, uzalendo, utaifa umesoma umepewa imani kubwa ya ofisi, huu si Utanzania na hii sio aina ya utumishi wa umma ambao tunautarajia," aliongeza.

Mtaka ameagiza kukamatwa na kufanyiwa upekuzi mfanyabiashara anayedaiwa kuwakopesha runinga 15 watumishi wa idara ya manunuzi ambazo zinadaiwa kuibiwa bila maandishi yoyote.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Wilfred Kyambile, alisema alipata taarifa juu ya kupotea kwa runinga hizo kutoka kwa katibu wa hospitali na kuomba taarifa ya maandishi ambayo ilionyesha kuibiwa tatu badala ya 15.

"Baadaye wakaja wakazitafuta wakarudisha, lakini tulivyopita kuangalia tukaona kuna tofauti ya maboksi hazifanani na zile ambazo zimekuja mwanzo," alisema na kuongeza kuwa:

" Wazo la kwanza la katibu la 15 ni sahihi lakini la tatu ni la walakini kidogo, tukamwandikia barua ofisa ugavi akaandika barua zake, alikiri uzembe wake na watu wake wa ofisini na utunzaji wa funguo."

Awali Ofisa Manunuzi wa Hospitali hiyo, Aloyce Kavumika, alimwambia mkuu wa mkoa kuwa alipokea runinga 36 zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 32 na kupata taarifa ya wizi huo akiwa safarini.

"Nilipigiwa simu na mkuu wa kitengo cha ubora akaniambia TV zinaibiwa huku, kontena liko wazi imekuaje? akaniambia amepigiwa simu na mlinzi baadaye tukaa na wenzangu tukakubaliana tukakope dukani ili tuzirudishe," alisema Kavumika.

Mlinzi wa Hospitali hiyo, Godwin Mtenzi, alisema wizi huo umetokea, lakini kontena hilo halikuvunjwa na badala yake kufuli lilifunguliwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga, alisema wamefungua jalada la uchunguzi kuhusiana na tukio hilo na kuahidi kutoa taarifa baada ya kukamilika..



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (katikati), pamoja na baadhi ya viongozi wa Wilaya ya Chunya wakiwa pamoja mwishoni mwa wiki na watoto wanne pacha waliozaliwa katika Zahanati ya Kijiji cha Sangambi wakati wa huduma ya mama na mtoto inaanzishwa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanne mbaroni uporaji pikipiki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani hapa linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kuwateka madereva wa bodaboda na kuwapora pikipiki zao.

Kamanda wa Polisi mkoani hapo, Benjamin Kuzaga, aliwataja wahuhumiwa hao kuwa ni Mandela Charles (28), Mkazi wa Iyunga Mapinduzi, Evaristo Marcus (37) wa Izuo, Emmanuel Razako (25) na Ibrahim Nelson (25) wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Kamanda Kuzaga alisema watuhumiwa hao walikamatwa katika misako iliyofanywa na makachero wa jeshi hilo katika maeneo ya Izuo na Mlima Iwambi.

Alisema watuhumiwa walipopekuliwa walikutwa na pikipiki tano zinazodhaniwa kuwa ni za wizi na baadhi ya vifaa vya vyombo hivyo vya moto, vikiwamo viti, kofia ngumu na vifaa vya kufungulia pikipiki.

"Tumewahoji na wamekiri kujihusisha na matukio ya wizi wa pikipiki katika maeneo mbalimbali ya Mji wa Mbalizi jijini Mbeya, Wilaya ya Rungwe na katika mkoa jirani wa Songwe," alisema.

Alisema watuhumiwa wanaendelea kuhojiwa ili kupata mtandao mzima wa wezi wa pikipiki na kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka.

Vilevile alisema jeshi hilo linashirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kubaini umiliki halali wa pikipiki hizo walizokutwa nazo watuhumiwa hao.

Kuzaga aliwataka wananchi walioibiwa pikipiki katika maeneo mbalimbali mkoani Mbeya na Songwe kufika katika Kituo cha Polisi cha Mbalizi kwa ajili ya kutambua mali zao.

# Serikali yasaka megawati 70 umeme Ngosi

**Na Nebart Msokwa,**
RUNGWE

SERIKALI imeanza kuchimba kisima cha kwanza kwa ajili ya kufanya utafiti wa kuzalisha umeme utokanao na jotoardhi pembezoni mwa Ziwa Ngosi wilayani hapa Mkoa wa Mbeya.

Akizungumza mbele ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Rungwe, Meneja Mkuu kupitia Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi nchini (TGDC), Mathew Mwangoba, alisema mradi ukikamilika utazalisha megawati 70 za umeme na kuingizwa kwenye gridi ya taifa.

Mwangoba, alisema kazi ya kufunga mtambo imekamilika na sasa uchimbaji wa kisima hicho utaanza wakati wowote na kufanyika kwa kati ya siku 40 hadi 45.

Alisema serikali imetoa Shilingi bilioni 20 kununulia mtambo huo na fedha nyingine zitaendelea kutumika kuchimba visima vingine vya utafiti katika eneo hilo la Ziwa Ngosi.

"Serikali imedhamiria kufanya utafiti wa kina utakaowezesha nchi yetu kuanza kuzalisha umeme utokanao na rasilimali ya jotoardhi, ndio maana sisi kama wataalamu tumepewa zaidi ya Shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kufanikisha azma hiyo na sasa tumeingia kazini," alisema Mwangoba ambaye kampuni yake ndiyo inayofanya kazi hiyo.

Alisema kwa kuanzia wanatarajia eneo hilo la Ziwa Ngozi litaanza kuzalisha umeme wa megawati tano kuanzia mwakani na kiwango hicho kitaendelea kuongezeka taratibu kulingana na taarifa za kitafiti hadi kufikia cha juu cha megawati 70.

Meneja Mradi huo, Mhandisi Fatumat Mzava, alisema wanatarajia kuchimba visima hivyo ili kufanikisha azma ya kuzalisha umeme katika eneo hilo.

Fatumat alisema mbali na kisima hicho kinachochimbwa katika Kata ya Isongole, vingine vitachimbwa kata za Swaya na Nsongwi Juu.

"Ukiangalia umbali kutoka kisima kimoja hadi kingine ni zaidi ya kilometa 20, hii itatusaidia kupata taarifa za kutosha za kisayansi ambazo zitatuwezesha kuzalisha umeme mwingi katika eneo hili," alisema.

Akizungumza baada ya kukagua mradi huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu, alisema mradi huo utakuwa na faida kubwa kwa wakazi wa Rungwe na Watanzania wote, hivyo unapaswa kulindwa na kuheshimiwa.

Haniu, alisema serikali inawekeza fedha nyingi katika uzalishaji wa umeme nchini ili kuwaondolea wananchi kero ya upatikanaji wa nishati hiyo na kuleta maendeleo nchini.

"Mradi huu ni wetu upo kwenye maeneo yetu, hivyo tunapaswa kuulinda ili utuletee tija kwenye maisha yetu, hatutamvumilia mtu yeyote atakayejaribu kuuhujumu," alionya.

Aliwataka wakazi wanaoishi kuzunguka mradi huo kutoa ushirikiano wao unapohitajika ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati na kuanza kutoa tija kwa Watanzania.

Diwani wa Kata ya Isongole, Mwalingo Sote, alisema wakazi wa eneo hilo wameanza kufaidi matunda ya mradi huo kwa Shule ya Msingio ya Isongole kupata huduma ya maji kwa kuwekewa tangi na wanafunzi kuondokana na kero ya kwenda mtoni kuteka maji kwani walikuwa wakihatarisha maisha yao kwa kuvuka barabara Kuu ya Tanzania- Malawi yenye magari mengi.



## Mradi wa umeme jadidifu waja Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar ( SUZA), Profesa Mohammed Makame Haji amesema Mradi wa Umeme wa Jua (DALILA) utasaidia kuongeza nishati jadidifu katika sekta ya nishati visiwani hapa.

Akizungumza jana wakati akifungua kongamano la wadau wa mradi huo katika Chuo cha Utalii Maruhubi visiwani hapa, alisema lina lengo la kutafuta njia ya kupata nishati ya umeme mbadala isiyotokana na nguvu ya maji, mifumo ya jua na ya upepo.

Alisema mradi huo utasaidia kukuza maendeleo ya nishati ya umeme wa jua nchini na kuwawezesha vijana kujifunza programu hiyo na kuwainua kiuchumi.

Hata hivyo, alisema kuanzishwa kwa mradi huo wa miaka mitatu kutasaidia kukiendeleza chuo hicho na wananchi kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Awali, alisema programu hiyo itawasaidia wananchi wanaotumia boti za umeme wa jua na kuimarisha sekta ya uchumi wa buluu.

Aliwataka vijana, taasisi binafsi na serikali kushirikiana kuendeleza mradi huo katika kazi zao.

Msimamizi wa mradi huo SUZA, Said Bakar, alisema unatarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya nishati ya umeme wa jua na kukuza uchumi wa wananchi na Taifa.

Aliiomba serikali kuweka maabara maalumu ya mradi wa nishati ya umeme wa jua ili kufanya kazi zake kwa uhakika.

Kongamano hilo limewashirikisha wataalamu, wanafunzi na walimu kutoka vyuo vikuu vya Uganda, Tanzania Bara na Zanzibar.

**Alisema mradi huo utasaidia kukuza maendeleo ya nishati ya umeme wa jua nchini na kuwawezesha vijana kujifunza programu hiyo na kuwainua kiuchumi.**

# Miswada sita kutikisa Baraza la Wawakilishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MISWADA sita ya sheria inatarajiwa kuwasilishwa katika mkutano wa 13 wa Baraza la 10 la Wawakilishi Zanzibar utakaoanza kufanyika kesho visiwani hapa.

Hayo yalisemwa jana na Katibu wa baraza hilo, Raya Issa Mselem, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake huko Chukwani nje ya mji wa Zanzibar.

Mselem, alisema miswada hiyo inayotarajiwa kuwasilishwa katika kikao hicho ni wa Sheria ya Mahakama ya Kadhi Namba 9 ya mwaka 2017 na kutunga sheria mpya pamoja na mambo mengineyo.

Alisema lengo la mswada huo ni kuongeza ufanisi wa Mahakama ya Kadhi kushughulikia masuala ya jamii ya Waislamu, ndoa, mirathi na matunzo ya watoto.

Aliutaja mswada mwingine kuwa ni wa sheria ya kufuta Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar namba 14 ya mwaka 2018 na kutunga Sheria ya Uwekezaji Zanzibar..

"Mswada huo unatarajiwa kuwasilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga kwa lengo la kuongeza ufanisi katika miradi ya uwekezaji inayosajiliwa na taasisi hiyo," alisema.

Hata hivyo, alisema katika kikao hicho, mswada wa kufuta sheria ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali namba 11 ya mwaka 2003 na kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Umma, unatarajiwa kuwasilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman.

Miswada mingine ni kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili ya Bahari Zanzibar, Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar kwa ajili ya ununuzi, utengenezaji na uhifadhi na usambazaji wa dawa.

Katibu huyo, alisema katika kikao hicho Mwakilishi mteule wa Jimbo la Mtambwe, Dk. Mohamed Ali Suleiman anatarajiwa kuapishwa baada ya kuibuka na mshindi katika uchaguzi mdogo uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Alisema maswali 88 yanatarajiwa kuulizwa na wawakilishi na kujibiwa na mawaziri wa wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).



Mkurugenzi wa Shule ya Msingi ya Montisori ya Zanzibar, Suzy Maziku (kushoto), akizungumza kwenye mahafali ya nne ya shule hiyo, Wilaya ya Magharibi juzi. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# 800 kulipwa fidia Uwanja wa Ndege Pemba

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) inatarajia kuanza kuwalipa zaidi ya wananchi 800 fidia ili kupisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, wakati akizungumza na viongozi na watendaji kutoka taasisi mbalimbali katika kikao maalumu kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa uwanja huo.

Dk. Saada alisema kuwa wananchi hao, wataanza kuingiziwa malipo yao ya fidia kwa awamu ya kwanza baada ya SMZ baada ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kukamilisha uhakiki kwa awamu hiyo ya kwanza.

Wakati huo huo; mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) wamefanya ziara katika Shehia za Mvumoni na Mfikiwa kisiwani Pemba kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi, kukagua maeneo na kuhakiki ulipaji fidia linavyoendelea.

Mawaziri hao ni Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, Ardhi, Maendeleo ya Makazi, Rahma Kassim Ali na Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili, Hamza Hassan Juma.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, walisema ziara hiyo ni utekelezaji wa ahadi ya SMZ kuwalipa wananchi fidia kabla ya ujenzi wa uwanja huo kuanza.

**Dk. Saada alisema kuwa wananchi hao, wataanza kuingiziwa malipo yao ya fidia kwa awamu ya kwanza baada ya SMZ baada ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kukamilisha uhakiki kwa awamu hiyo ya kwanza.**

Walisema kuna changamoto ndogo zilizojitokeza na kuahidi kuzichukua kwa ajili ya kuzifanyia kazi.

Ujenzi huo wa uwanja unatarajiwa kukifungua kisiwa hicho kiuchumi kwa ndege kutoka mataifa mbalimbali duniani kushusha abiria kisiwani hapo, wakiwamo watalii.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**IVO SOSTHENES BENARD** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S5198/0058** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ANNA TIBAIJUKA SEKONDARI** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/46094/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOSIAH OMBENI ASSERY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0198/0057** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **AILANGA LUTHERAN JUNIOR SEMINARY** mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/PWA/KIB/3708/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**VERONICA MASULE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0630-0045** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NYEGINA SEKONDARI mwaka 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/2825/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACKSON S. LIBABA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0549-0140 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia LUGOBA SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/38313/2023**.

## KUPOTEA KWA VYETI



**SAFIA FRANK NGOWI** anatangaza kupotea kwa cheti cha darasa la saba chenye Admission No. 025 kilichotolewa na Debora Primary School mwaka 2008. Cheti cha kidato cha nne chenye index number S1009-0060 kilichotolewa na Babati Day Sekondari mwaka 2012. Cheti cha chuo Diploma in Animal Health chenye namba DAHP/05/392/2015 kilichotolewa na Chuo cha LITA MADABA mwaka 2015. Yeyote atakaye viona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MZZ/RB/1126/2023.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **WITNESS ZACHARIA IHEMULA** anatangaza kupoteza kadi ya gari aina ya Noah lenye namba za usajili **T866DFL** yenye majina ya **FORTUNATUS BINAMUNGU DAUDI**. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **PHQ/KAG/BUK/3452/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0756-751929 au 0710-399431.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAMADHANI SAID ATHUMANI,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Toyota Corona yenye Model No AT211, No za Usajili **T 841BJU,** CHASSIS NO **AT2110105955,** ENGINE **NO AT211.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/10002/2023**

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA.

**VIVIAN SULEIMAN NYAMBUI** ANATANGAZA KUPOTELEWA KWA OFA YA KIWANJA NAMBA 430 BLOCK FF NYAKATO. OFA HII ILIPOTEA KWENYE GARI.

KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KATIKA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAYE.

TAARIFA YA POLISI: **PHQ/MWA/NYA/8367/2023.**

## KUPOTELEWA NYARAKA YA UMILIKI KIWANJA

**Paulina Bundala Muhende** Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu Roza Laurent Thomas Anatangaza kupotelewa na Nyaraka ya Umiliki wa Kiwanja namba 244 Kitalu "Y1"(HD) kilichopo Ibinzamata Manispaa ya Shinyanga

Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Paulina kwa simu namba **0744-690676.**

Taarifa ya Polisi RB: **PHQ/SHI/SHI/1126/2023.**

**DEED POLL ON CHANGE OF NAME**
**REGISTRATION OF DOCUMENT ACT**
**(Cap.117 R.E 2002)**

THIS DEED is made this 20th day of October, 2023 at MANUNDU KOROGWE

BY THIS DEED, I the undersigned and the person with the name of SHOSE L. KAAYA P.o Box National Housing, Korogwe, a Citizen of the United Republic of Tanzania by Birth DO HERE BY ABSOLUTELY renounce and abandon the use of my former names of SHOSE SIMONI SALVANO as it appear to my NIDA NA. 19520917-21601-00001-12 and SHOSI L. KAAYA as it appear to my letter of Retirement on date 27th, MARCH,2012.

And in pursuance of such change of as name aforesaid I HERBY DECLARE that i shall all times hereafter in all records, deeds and instruments in writting and in all action and proceeding and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever related to my business use and sign the said name of SHOSE L. KAAYA as it appear in my NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND as my name in lieu of the said name SHOSE SIMONI SALVANO renounce as foresaid.

And I hereby authorize and request all people to designate and address me by such assumed name of SHOSE L. KAAYA Only.

IN WITNESS WHEREOF I have hereunder signed my assumed name SHOSE L. KAAYA and have set my hand this 20th , Day of October, 2023.

SIGNED AND DELIVERY by the said,
SHOSE L. KAAYA
Who is known to me personally/identified
To me by.........
This 20th DAY OF October, 2023

SHOSE L. KAAYA



BEFORE ME:-
..........................
COMMISSIONER FOR OATH
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MANUNDU - KOROGWE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA 213/2023**

**MDAI:TWILUMBA GROUP**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: HALIMA SELEMANI**

**KWA; HALIMA SELEMANI WA AZIMIO KIHOLO MOROGORO**

**OMBI LA MDAI : TWILUMBA GROUP**
**KATA YA KIHONDA MAGOROFANI**
**MADAI YA:213/2023**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri lilimepangawa kusikilizwa mnamo tarehe 30 Mwezi 11 Mwaka 2023 saa Asubuhi/alasiri.

Angalia kama hukudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii inaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe mwezi 2023.

..............................
**HAKIMU**
**MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**MOROGORO**

---

**FOMU MIRATHI - 3**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya RUFIJI**
**Kituo cha IKWIRIRI Mkoa wa PWANI**
**Shauri la Ndoa Na. 32/2023**
**Jina la Mdai SARAH GODSON MSHEWA**
**Jina la Mdawia DAVID CHACHA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

Kwa: DAVID CHACHA
MARA MUSOMA
Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba
MADAI YA KUVUNJA NDOA/TALAKA/MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA WATOTO

Kwahiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 6 Mwezi 12 Mwaka 2023 saa 1:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 22 Mwezi 11 Mwaka 2023.

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI**

**SHAURI LA TALAKA 07/2023**

**SHAKIRA AMON GAVILE..........................MDAI**

**MARCO EMMANUELMPOGOLE.............MDAIWA**

Unatakiwa kufika Mahakamani tarehe 05/12/2023 saa 2:30 asubuhi kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu

Usipofika shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa maamuzi.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama leo hii tarehe 14/11/2023.

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO
IRINGA MJINI

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0745 700 710.
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

ISRAEL DHIDI YA HAMAS

# Operesheni ya kijeshi yarejea Gaza

**Gaza City,** GAZA

WAZIRI Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu amesema alimwambia Rais Joe Biden kwa njia ya simu kwamba, Israel itaanza upya shughuli zake huko Gaza kwa nguvu kamili mara tu mapatano ya sasa yatakapokamilika.

Israel ilisitisha operesheni zake huko Gaza, siku ya Ijumaa, ili kuruhusu mateka waliokuwa wakizuiliwa katika eneo hilo kuachiliwa na pia wafungwa wa Kipalestina kuruhusiwa kuondoka kutoka magereza ya Israel lakini mapatano hayo yalitarajiwa kudumu hadi jana.

Netanyahu aliongeza kuwa atakaribisha kurefushwa kwa mapatano hayo, ikiwa itamaanisha kuachiliwa kwa mateka 10 zaidi kila siku, kama ilivyoainishwa katika makubaliano ya awali.

Ikulu ya White House ilisema viongozi hao wawili wamekubaliana kwamba wataendelea kufanya kazi, ili kuhakikisha kuachiliwa kwa mateka wote.

Wizara ya Afya ya Gaza inayoongozwa na Hamas, imesema zaidi ya watu 14,500, wakiwamo watoto wasiopungua 5,500, wameuawa huko Gaza tangu Israel ilipoanza kushambulia eneo hilo kwa kulipiza kisasi mashambulizi ya Oktoba 7, mwaka huu.

Mashirika ya Umoja wa Mataifa yanasema, wizara hiyo inatoa takwimu za kuaminika. Hamas pia imeonyesha nia ya kutaka kuzidishwa kwa muda wa kusistishwa kwa mapigano huku Jordan ikitaka makubaliano ya kudumu ya kumaliza vita kuafikiwa. **BBC**



## Sierra Leone yarejea katika utulivu

**Freetown,** SIERRA LEONE

RAIS wa Sierra Leone Julius Maada Bio (pichani chini) amesema hali ya utulivu imerejea nchini humo, baada ya kutokea shambulizi dhidi ya kambi ya jeshi kwenye mji mkuu wa taifa hilo mapema juzi.

Akilihutubia taifa kupitia televisheni usiku wa kuamkia jana, rais Bio alisema wote waliopanga na kuongoza shambulizi hilo wamekamatwa na kwamba operesheni za usalama na uchunguzi wa suala hilo vinaendelea.

"Viongozi karibu wote waliokula njama ile wamekamatwa. Operesheni za usalama na uchunguzi zinaendelea," alisema rais Bio katika hotuba yake na akiongeza kuwa serikali yake itahakikisha wote waliohusika wanawajibishwa.

Mwandishi wa habari wa AFP ameripoti kuwa, utulivu ulianza ukirejea polepole katika mji mkuu kufikia Jumapili jioni, lakini vituo vya upekuzi vilivyo na ulinzi mkali wa vikosi vya usalama bado vimesalia.

"Serikali inao udhibiti kamili wa hali ya usalama mjini Freetown, washambuliaji wanajisalimisha," Waziri wa Habari, Chernor Bah aliiambia AFP kabla ya hotuba ya Rais Bio.

Video zilizochapishwa kwenye mitandao ya kijamii, zimewaonyesha wanaume waliovalia sare za kijeshi wakiwa wamekamatwa na kuwekwa ama kando au ndani ya malori ya kijeshi. **DW**



## UAE yashangaza kunadi utajiri wake COP28

**Abu Dhabi,** U.A.E

UMOJA wa Falme za Kiarabu (UAE), ulipanga kutumia nafasi yake kama mwenyeji wa mazungumzo ya mabadiliko ya tabianchi ya Umoja wa Mataifa (UN), kama fursa ya kufanya mikataba ya mafuta na gesi.

Nyaraka za muhtasari zilizovuja zinaonyesha mipango ya kujadili mikataba ya mafuta na mataifa 15.

Baraza la Umoja wa Mataifa linalohusika na mkutano huo wa COP28, liliwaambia BBC wenyeji wanatarajiwa kuchukua hatua bila upendeleo au maslahi binafsi.

Timu ya UAE haikukataa kutumia mikutano ya COP28 kwa mazungumzo ya biashara na ilisema mikutano ya faragha ni ya faragha.

Ilikataa kutoa maoni juu ya kile kilichojadiliwa katika mikutano na kusema kazi yake imekuwa ikilenga hatua ya maana ya mabadiliko ya tabianchi.

Nyaraka hizo zilizopatikana na waandishi wa habari wa kujitegemea katika Kituo cha Taarifa za Hali ya Hewa, wanaofanya kazi pamoja na BBC, zilitayarishwa na timu ya UAE COP28 kwa mikutano na takribani serikali 27 za kigeni kabla ya mkutano wa kilele wa COP28, utakaoanza tarehe 30 Novemba.

Ilijumuisha mazungumzo yaliyopendekezwa, kama vile ya China ambayo inasema Adnoc, kampuni ya mafuta ya UAE, iko tayari kutathmini kwa pamoja fursa za kimataifa za LNG (gesi asilia), nchini Msumbiji, Canada na Australia. **BBC**

## WHO yaeleza wasiwasi kuhusu Monkeypox

**Nairobi,** KENYA

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limeeleza wasiwasi wake kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa Monkeypox nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Zaidi ya watu 581 wamefariki kutokana na ugonjwa huo.

WHO sasa inahofia kuwa iwapo hali hiyo haitadhibitiwa, huenda mataifa jirani pia yakaathirika. Wagonjwa zaidi ya 13,000 wameripotiwa kuugua ugonjwa huo wa Monkeypox, mamlaka za afya nchini humo zikihusisha ukosefu wa pesa kuwa chanzo kikuu cha kusambaa kwa ugonjwa huo kwa kasi.

Ugonjwa huo umeathiri mikoa 21 kati ya 26 nchini DRC, mikoa ya Équateur, Sankuru, Mai-Ndombe na jiji la Kinshasa ikiathirika ziadi.

Ofisa wa Serikali ya Kinshasa anayehusika na hali ya dharura, Cris Kasita, amesema serikali inahitaji Dola millioni nne, kukabili hali ya ugonjwa huo katika mikoa mine iliyoathirika zaidi. **RFI**

# KENGOLD, MBEYA KWANZA, TMA, NI VITA KALI YA KUPANDA LIGI

**Na Adam Fungamwango**

HII unaweza ukasema kuwa ni vita ya kupanda Ligi Kuu ambayo inapiganwa kwenye Ligi ya Championship, kwani baada ya Ijumaa Mbeya Kwanza kukaa kileleni kwa kuichapa Cosmopolitan fc mabao 3-2, juzi kibao kimegeuka kwa Kengold kupindua meza na kukaa juu ya msimamo kwa kuifunga Mbuni FC bao 1-0 mechi ikichezwa Uwanja wa Sokoine, Mbeya, huku timu tatu za juu zote zikiwa zimefungana pointi.

**Timu za Kengold, Mbeya Kwanza na TMA zote sasa zina pointi 26, na kutengeneza vita kali ya kuwania kupanda Ligi Kuu msimu ujao.**

KenGold inaongoza ligi kuanzia juzi ikiwa na pointi hizo, lakini imepachika mabao 20 na kuruhusu sita.

Mbeya Kwanza ambayo iliongoza kwa muda imeshuka hadi nafasi ya pili ikiwa pia na pointi 26, lakini ina mabao 19, ikiruhusu 11 kwenye wavu wake, huku TMA ikiwa nafasi ya tatu kwa pointi kama hizo, lakini yenyewe imefunga mabao 10, pia ngome yake inaonekana kuwa ngumu kwa kufungwa mabao mawili tu hadi kufikia raundi ya 12 ya ligi hiyo.

Pamba FC iko nafasi ya nne kwa pointi 24 na Mbuni ni ya tano na pointi zake 21, Biashara United ya sita na idadi kama hiyo ya pointi, Mbeya City ya saba pointi 18 na Polisi Tanzania ya nane ikikusanya pointi 17.

Timu ya Ruvu Shooting ambayo ilishuka daraja msimu uliopita, ipo hatarini kushuka Daraja la Pili (First League), kwani inaburuza mkia ikiwa na pointi moja tu mpaka sasa kwa michezo 12 iliyocheza.

## SHIDA IPO WAPI?...



Viongozi wa Klabu ya Simba, wakizungumza na wachezaji wa timu hiyo katika kikao maalum kilichofanyika baada ya mechi ya Kundi B ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas kumalizika kwa sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Jumamosi iliyopita. **PICHA: SIMBA**

# *Kuogelea Taifa warudi na makombe, medali*

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Timu ya Taifa ya Tanzania ya mchezo wa Kuogelea, limewapongeza wachezaji wake baada ya kufanikiwa kushika nafasi ya pili kwenye mashindano ya 8 ya Kanda ya Tatu (8th Africa Aquatics Zone 3 Swimming Championships), yaliyomalizika Novemba 25, mwaka huu, Kigali nchini Rwanda.

Mbali na ushindi huo Tanzania imepata medali 127 pamoja na makombe nane waliyoyapata wachezaji kwenye nafasi mbalimbali walizoshinda.

Akizungumza na Nipashe baada ya kuwasili nchini, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Alexander Mwaipasi, alisema wachezaji wake wameonesha juhudi kubwa licha ya changamoto mbalimbali walizozipata kutokana na aina ya mabwawa waliyokuwa wakiyatumia.

"Tanzania kushika nafasi ya pili ni mafanikio makubwa kwetu, wachezaji wangu wameonesha juhudi kubwa licha ya kuwapo kwa changamoto ya mabwawa tuliyokuwa tunayatumia," alisema Mwaipasi.

Aliongeza kuwa wapo kwenye mchakato wa kuwainua wasichana wenye umri kuanzia miaka 17 na kuendelea ili ipatikakane timu ya taifa yenye wasichana wengi wenye umri huo.

Alisema baada ya kuwasili atawapa wachezaji wake mapumziko ya muda mfupi na kurejea kambini wachezaji saba kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya vijana yatakayofanyika hivi karibuni nchini Mauritius.




Wakati huo huo Mwenyekiti wa Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA), David Mwansyoge, alisema amefurahishwa na matokeo hayo na kuwaomba wadau mbalimbali kuendelea kuwapa ushirikiano.

Nchi zilizoshiriki katika mashindano hayo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Eswatini, Rwanda, Eritrea, Djibouti, Afrika Kusini, Ethiopia pamoja na Burundi.

# JKU yajiimarisha kileleni msimamo wa Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kuendelea kuchanga karata zake vema kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, Maafande wa Klabu ya JKU, ushindi wanaoupata unakwenda sambamba na malengo yao kuhakikisha wanashinda michezo mitatu iliyobaki ya mzunguko huu wa kwanza.

Vinara hao wa Ligi Kuu Zanzibar hapo juzi waliibuka kidedea baada ya kutoka na ushindi mwembamba wao bao 1-0 dhidi ya Wanajeshi wa Kipanga FC katika muendelezo wa ligi hiyo, huo ukiwa ni mchezo wa mzunguko wa 12.

Kwa matokeo hayo JKU SC sasa imefikisha alama 29 ikiwabwaga wapinzani wao, KVZ ambao wapo nafasi ya pili na alama zao 23, Zimamoto FC pointi 23 pamoja na Kipanga FC ambao wenyewe wana alama 21 timu zote zikiwa tayari zimecheza michezo 12.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa JKU, Salum Ali, alisema katika mchezo wao huo ambao ndio ulikuwa mgumu zaidi ya mingine waliocheza, lakini walifanikiwa kupata alama tatu ambazo zimewafanya kuimarika zaidi kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu.

Alisema katika muendelezo wa kupata matokeo mazuri kwenye michezo ya Ligi Kuu Zanzibar, pongezi zote zinastahili kwenda kwa wachezaji na viongozi wa JKU kwa ari kubwa waliyokuwa nayo ya kuhakikisha wanacheza vizuri kila mchezo.

"Ushindi huu unachangiwa na wachezaji wenyewe kwa kujituma kwao ili kuhakikisha hatupotezi mchezo, bado ligi ni ngumu na kufanya vizuri mzunguko huu haimaanishi kama tushajihakikishia ubingwa, bado tunahitaji juhudi na hamasa ili tufanye vizuri zaidi," alisema.

Aidha, alisema hivi sasa wanandelea na maandalizi ya mchezo wao wa 13 ambao watashuka dimbani Desemba 3, mwaka huu, dhidi ya Malindi SC.

Aliendelea kuwaomba mashabiki wa JKU kujitokeza kwa wingi katika michezo yao ili kuhakikisha wanatoa hamasa kubwa itakayowafanya wachezaji kuwa na ari ya kupata matokeo mazuri.



HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### OSIMHEN MLENGWA MKUU

CHELSEA inatazamiwa kumfanya mshambulizi wa Napoli, Victor Osimhen kuwa mlengwa wao mkuu Januari, huku mshambuliaji huyo wa Nigeria mwenye umri wa miaka 24, akiwa tayari kuhamia Stamford Bridge. ***(Telegraph)***

### LINO AWINDWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inafuatilia kwa karibu ustawi wa winga wa Atletico Madrid, Samuel Lino mwenye umri wa miaka 23. ***(Todo Fichajes)***

### JUVE YATAKA NYOTA EPL

KLABU ya Juventus ina nia ya kusajili kiungo wa kati Januari na wana wachezaji watatu wa Ligi Kuu England kwenye orodha yao fupi - mchezaji wa Kimataifa wa Arsenal raia wa Ghana, Thomas Partey, 30, mchezaji wa Kimataifa wa Manchester City, Kalvin Phillips (27) na mchezaji wa Kimataifa wa Denmark na Tottenham Hotspur, Pierre-Emile Hojbjerg, 28. ***(Foot Mercato)***

### BARCO ATAKIWA MAN CITY

KLABU ya Manchester City inataka kumsajili beki wa pembeni wa Boca Juniors, Valentin Barco, kabla ya kumtoa kwa mkopo Leicester City, kinda huyo wa Kimataifa wa Argentina wa chini ya umri wa miaka 20. ***(Sun)***

### DE GEA ATAJWA SAUDIA

KLABU ya Saudia, Al-Ettifaq inaongoza jitihada za kutaka kumsajili kipa wa Hispania, David de Gea, 33, Januari. Mchezaji huyo yupo huru baada ya kuondoka Manchester United mwishoni mwa msimu uliopita. ***(Sun)***

### SANUSI KUTUA WEST HAM

KLABU ya West Ham inashughulikia mpango wa kumsajili beki wa kushoto wa FC Porto raia wa Nigeria, Zaidu Sanusi, 26. ***(Team Talk)***

### BAZUNU ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inafuatilia maendeleo ya mlinda mlango wa Southampton raia wa Jamhuri ya Ireland, Gavin Bazunu, 21. ***(Football Insider)***

### NUNEZ FEDHA ZAIDI

KLABU ya Liverpool inapaswa kuilipa Benfica pauni milioni 8.5 za ziada kwa Darwin Nunez, 24, baada ya mshambuliaji huyo wa Uruguay kucheza mechi yake ya 60 katika klabu hiyo dhidi ya Manchester City Jumamosi. ***(Mirror)***

### AKPOM AULIZIWA PALACE

CRYSTAL Palace na Fulham zimeulizia kuhusu mshambuliaji wa Ajax, Chuba Akpom, 28. ***(Team Talk)***


### GRAHAM SAFI EVERTON

KLABU ya Everton imekubali mkataba wa kumsajili mshambuliaji wa Linfield raia wa Ireland Kaskazini, Braiden Graham, 16. ***(Belfast Telegraph)***

### L. CITY KUMFUATA QUANSAH

KLABU za Leicester na Preston zinataka uhamisho wa mkopo Januari kumnunua beki wa Liverpool mwenye umri wa chini ya miaka 21, Jarell Quansah. ***(Alan Nixon kupitia Leicestershire Live)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# TEN HAG AKATAA KUMLINGANISHA GARNACHO NA ROONEY, RONALDO

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amepuuza ulinganisho uliofanywa kati ya Alejandro Garnacho na magwiji wa Manchester United, Wayne Rooney na Cristiano Ronaldo.

**Garnacho alifunga mkwaju wa ajabu wa juu na kuipa Man United uongozi wa mapema katika ushindi wao wa 3-0 dhidi ya Everton kwenye Ligi Kuu ya England katika Uwanja wa Goodison Park, Jumapili.**

Bao hilo limelinganishwa na mikwaju ya juu iliyopigwa na Wayne Rooney - kwa 'Mashetani Wekundu' hao dhidi ya Manchester City na Cristiano Ronaldo kwa Real Madrid dhidi ya Juventus kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya - mabao mawili ambayo yanachukuliwa kuwa bora zaidi ya tiktaka.

**●●● Usilinganishe, nadhani si sawa, wote wana utambulisho wao, anapaswa kufanya kazi...**

Hata hivyo, akizungumza na waandishi wa habari baada ya ushindi huo, kocha Ten Hag alikataa ulinganifu kati ya Garnacho na washambuliaji hao, akisisitiza kwamba kijana huyo anahitaji kufanya zaidi ikiwa anataka kuwa "mchezaji kama Rooney au Ronaldo."

"Usilinganishe, nadhani si sawa. Wote wana utambulisho wao. Ili Garnacho aende hivyo, ana mengi yanakuja, anapaswa kufanya kazi kwa bidii na kuifanya kwa msingi thabiti.

"Si mara ya kwanza kuona haya, mara nyingi tunaona mambo machache, lakini ukitaka kuwa mchezaji kama Rooney au Ronaldo, lazima ufunge mabao 20, 25 kwenye Ligi Kuu England.

"Si rahisi kupata, lazima ufanye bidii sana na uende katika njia ambazo zinaumiza. Mengi yanakuja, lakini uwezo anao.

"Lilikuwa bao la ajabu. Katika msimu, bado kuna michezo mingi ya kucheza, lakini labda tayari bao la msimu. Si tu kumaliza, ilikuwa nyuma hadi mwisho. Lakini umaliziaji ulikuwa wa kushangaza."

Bao hilo lilikuwa la pili kwa Garnacho katika mashindano yote kufikia sasa msimu huu, na atakuwa na matumaini ya kuongeza idadi hiyo wakati yeye na Manchester United watakapomenyana na Galatasaray katika mchezo muhimu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kesho.

# BARCELONA YAKANUSHA GUNDOGAN KUONDOKA




**BARCELONA,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Xavi Hernandez, amekanusha taarifa kwamba kiungo wake, Ilkay Gundogan, yupo njiani kuikacha timu hiyo na kuelekea Saudi Arabia.

Xavi ameeleza hayo alipozungumza na vyombo vya habari kuwa mchezaji huyo ataendelea kuwapo ndani ya Barcelona hadi mwishoni mwa msimu wa 2023/2024.

Kocha huyo alifafanua kuwa hii si mara ya kwanza kwa Gundogan kuhusishwa na kutaka kuondoka klabuni hapo, kwani anaamini huo ni mpango wa kutaka kuvuruga mambo ndani ya klabu hiyo.

"Nimepata habari Gundogan anaenda kucheza soka Saudi Arabia, hili halipo ni uzushi tu," alisema Xavi.

"Amewahi kuhusishwa kwenda Real Madrid, najua kuna wakati alikuwa hana furaha ndani ya Barca, lakini huo ni uzushi kwamba anaenda Saudi Arabia."

Kauli hiyo, imekuja baada ya gazeti la Asharg To the-Awsat kueleza kuwa mchezaji huyo wa Ujerumani amefungua mlango wa mazungumzo na Klabu za Saudi Arabia.

Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Saudi Arabia, Saad To the-Ladhim, amethibitisha kuwa mchezaji huyo huenda akatua nchini humo.

Habari zaidi zinaeleza kuwa mchezaji huyo huenda akatua ndani ya timu moja wapo kati ya Al Nassr au Al Ittihad.

# Newcastle kutupa ndoano Saudia

**NEWCASTLE,** England

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe, amekiri klabu hiyo huenda ikasajili wachezaji kutoka Saudi Arabia Januari 2024, ili kuboresha kikosi chake ambacho kina wachezaji wengi majeruhi.

Lakini bosi huyo wa Magpies alisema ni "ajabu" Newcastle ndio inatolewa macho zaidi kwenye usajili baada ya klabu za Ligi Kuu England kupigwa marufuku usajili wa mkopo kutoka Saudi Arabia itakapofika Januari 2024.

Hiyo inamaanisha Newcastle itakuwa huru kusajili wachezaji kutoka klabu za Saudi Arabia ambayo pia inamilikiwa na Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi Arabia.

Newcastle inatazamia kufanya usajili wa kiungo wa zamani wa Wolves, Ruben Neves ambaye amejiunga na Al-Hilal kipindi cha usajili wa majira ya joto.

Al-Hilal ni moja ya timu inayosimamiwa na Mfuko wa Uwekezaji wa Umma pamoja na Al-Nassr, Al-Ittihad na Al-Ahli, na wanamiliki mastaa kama Cristiano Ronaldo, NGolo Kante na Riyad Mahrez.

Kutokana na wachezaji wake wengi kuwa majeruhi kocha huyo anataka kulazimisha usajili dirisha dogo kwani kukosekana kwa Sandro Tonali ambaye amefungiwa miezi 10 baada ya kukutwa na hatia ya kucheza kamari, wachezaji kama Sven Botman, Callum Wilson, Harvey Barnes, Dan Burn, Jacob Murphy, Matt Targett na Elliot Anderson wataendelea kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu.



# Kocha wa zamani England afariki dunia

**LONDON,** England

KOCHA wa zamani wa England, Terry Venables, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 80.

Venables alikuwa usukani kwenye kampeni ya kukumbukwa ya England kwenye Euro 1996 na alifurahia mafanikio katika ngazi ya klabu akiwa na Barcelona, Tottenham Hotspur na Leeds United.

Familia ya bosi huyo mashuhuri ilithibitisha habari hizo Jumapili wakati wa chakula cha mchana.

Taarifa ilisomeka hivi: "Tumehuzunishwa sana na msiba wa mume na baba mzuri ambaye alifariki dunia kwa amani jana baada ya kuugua kwa muda mrefu. Tungeomba faragha itolewe wakati huu wa huzuni ili kuturuhusu kuomboleza kifo cha mtu huyu mzuri ambaye tulikuwa na bahati sana kuwa naye maishani mwetu."



Akiwa mchezaji, Venables alifanikiwa kuichezea Chelsea na kucheza zaidi ya mechi 200 katika klabu hiyo, kabla ya kuichezea Tottenham Hotspur na QPR.

Kazi yake ya kuvutia na Crystal Palace ilisababisha Barcelona kuja kupiga simu mwaka 1984 ambapo alipata jina lake la utani maarufu la 'El Tel'.

Venables aliiongoza Barca kutwaa taji la LaLiga na fainali ya Kombe la Ulaya katika miaka yake mitatu pale Katalunya, lakini aliondolewa mwaka 1987, kabla ya kuhamia Tottenham.

Alinyanyua Kombe la FA Kaskazini mwa London na kufikia 1994, Venables alikuwa ameajiriwa na FA kuchukua kazi kubwa zaidi ya kuwa kocha wa England.

Timu yake ya Euro 96 ilifika nusu fainali kabla ya kupoteza kwa Ujerumani kwa mikwaju ya penalti kwenye Uwanja wa Wembley.

Gary Lineker, ambaye alicheza chini ya Venables kule Barcelona, alikuwa mmoja wa watu wa kwanza kutoa pole kwa bosi wake wa zamani.

Lineker aliandika kwenye X (zamani Twitter): "Nimehuzunishwa kusikia kwamba Terry Venables amefariki. Kocha bora na mbunifu ambaye nilipata fursa na furaha kucheza chini yake. Hata hivyo, alikuwa zaidi ya kocha. Alikuwa mchangamfu, alikuwa mjanja, alikuwa rafiki. Atakumbukwa sana. Kutuma upendo na rambirambi kwa familia."

Spurs walithibitisha kwa kutoa heshima kwa Venables kabla ya mechi ya juzi dhidi ya Aston Villa.

# SHABIKI AMPIGA REFA, TIMU YAPOKWA POINTI NA FAINI JUU

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KAMATI ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ligi ya Bodi ya Ligi Zanzibar, imetoa alama tatu na mabao mawili kwa Zimamoto SC baada ya shabiki wa timu ya Kundemba FC kumpiga mwamuzi pembeni (mshika kibendera namba mbili) na kusababisha mchezo huo kuvunjika ndani ya dakika za nyongeza.

**Katika mchezo huo uliochezwa Novemba 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Mau hadi unavunjika timu hizo zilikuwa zimetoshana nguvu kwa kufungana mabao 2-2.**

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na kamati hiyo na kutiwa saini na Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Issa Kassim, imeeleza kuwa maamuzi hayo yaliyotolewa ni kwa mujibu wa Kanuni ya Mashindano ya ZFF sura ya 20 (6) na sura ya 27 (1) (2) (3), (i), (ii) na (4).

Taarifa hiyo ilieleza kuwa mbali na adhabu hiyo, timu ya Kundemba FC imepigwa faini ya Sh. milioni tano ambapo Sh. milioni moja ni kwa sababu ya kufanya fujo zilizosababisha kuvunjika mchezo huo na Sh. milioni nne, ametozwa shabiki wake aliyemshambulia mwamuzi wa mchezo huo.

Aidha, wachezaji wa timu ya Kundemba FC, Ally Makame, amefungiwa mechi tatu, huku Issa Ramadhani akifungiwa mechi moja kwa kufanya vitendo vya utovu wa nidhamu katika mchezo huo.

Hata hivyo, kamati hiyo ambayo ipo chini ya Bodi ya Ligi Zanzibar, imeipa siku saba timu ya Kundemba FC kuhakikisha inalipa faini hizo.

WAYA...




Winga wa Manchester United, Alejandro Garnacho, akibinjuka kuifungia timu yake bao la kwanza katika dakika ya tatu, wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Everton, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa juzi usiku katika Uwanja wa Goodison Park. **PICHA: MTANDAO**

## Kocha Bara U-18 atamba mvua imeinusuru Uganda

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wavulana ya Tanzania Bara chini ya miaka 18, Habib Kondo (pichani), amesema bila ya kunyesha mvua kipindi cha pili, Waganda wangeoga magoli mengi katika mechi ya juzi kwenye Uwanja wa Bukhungu, Kakamega nchini Kenya wakishinda bao 1-0.

Katike mechi hiyo ya ufunguzi wa michuano ya Kombe la Afrika Mashariki na Kati, CECAFA kwa vijana wa umri huo, ambayo mwaka huu yanafanyika nchini Kenya, bao pekee lilifungwa dakika ya 15 na Sharif Wilson.

Kocha huyo amesema kitu pekee ambacho kiliiokoa Timu ya Taifa ya Uganda ni mvua ambayo iliwalazimisha kubadili aina yao ya uchezaji.



"Kwanza tunashukuru kwa kupata matokeo ya ushindi kwenye mechi ya leo (juzi), tulijua mechi ingekuwa ngumu, na kweli, mwanzoni tulipanga 'plani' yetu lakini kwa bahati mbaya mvua ilitibua kila kitu.

"Sisi tulijiandaa kutawala mpira, lakini huwezi kufanya vile kama kuna mvua, uliona kipindi cha kwanza tulivyocheza, tulianza vizuri tu, lakini kipindi cha pili ilipokuja mvua hali ilibadilika, ikabidi sasa mfumo nao ubadilike," alisema kocha huyo.

Hata hivyo, amesema ushindi walioupata ni muhimu kwani utasababisha wajiamini kuelekea katika mechi inayofuata.

Bara iko Kundi B na timu ndugu zao Zanzibar, Sudan Kusini na Uganda, mechi zake zikichezwa Kakamega, huku Kundi A likiwa na Kenya, Somalia, Rwanda na Sudan ambalo kituo chake ni Kisumu.

Ratiba inaonesha kuwa kesho, Bara itacheza mechi yake ya pili dhidi ya Sudan Kusini na Zanzibar itakipiga dhidi ya Uganda.

## *Jwaneng, Wydad kuamua hatima*

INATOKA UKURASA 24

wamekiri kukosea na kudai sasa wanafungua ukurasa mpya wa kupambana na kupigania nembo ya klabu hiyo kuhakikisha wanafikia malengo yanayotarajiwa na Wanasimba.

Nyota hao, wakiongozwa na kiungo Clatous Chama, aliwaomba msamaha mashabiki wa timu hiyo kwa matokeo ya mechi tatu zilizopita kwa kutocheza vizuri na hawakustahili kupata matokeo hayo.

Simba ilipoteza mechi dhidi ya Yanga kwa mabao 5-1, ikatoka sare ya ba 1-1 na Namungo FC kwenye Ligi Kuu, kabla ya kupata tena sare kama hiyo dhidi ya Asec Mimosas Ligi ya Mabingwa Afrika.

Chama alisema baada ya matokeo ya mechi yao na Asec Mimosas walikaa, wakajiuliza na kuona makosa yao, hivyo watauhakikisha haitajirudia tena.

"Hakuna ugomvi kati ya uongozi na wachezaji, ni upepo mbaya umepita kwetu, tukumbuke msimu uliopita tulipoteza dhidi ya Horoya FC ugenini na Raja Casablanca hapa nyumbani, lakini tulitulia na kufanya vizuri hadi kufika robo fainali Ligi ya Mabingwa," alisema Chama na kuongeza:

"Simba ni timu kubwa na matarajio yake ni kufanya vizuri kila mashindano ili kufikia malengo, tumepitia katika kipindi kigimu, kama timu, hatupaswi kuonyesheana vidole badala yake tuwe pamoja na hatimaye tuvuke na kurejea katika kipindi cha furaha."

## Gamondi ataka nidhamu kuivaa Al Ahly Jumamosi

INATOKA UKURASA 24

ezo ni kitu muhimu na hasa unapocheza na timu kubwa na bora hata Afrika, katika mechi iliyopita tumefungwa mabao 3-0 kilichotugharimu ni nidhamu ya mchezo, makosa machache tu ukiyafanya kwa timu kama hizo wanakuadhibu.

"Unaweza usipate adhabu au kujua kama umefanya makosa kama ukicheza na timu za kawaida, hasa nyingi za Ligi Kuu na si hizi kubwa na kwa mara nyingine tena tunakwenda kucheza mechi nyingine kubwa na bora Afrika, tusahau yaliyopita tuangalia tutakabiliana nao vipi," alisema kocha huyo.

Alibainisha kuwa katika mechi ijayo atawatengeneza wachezaji wake wacheze kwa umakini, nidhamu kubwa na kutofanya makosa madogo madogo kama yale ya mechi iliyopita.

"Ninawapa mbinu ya kucheza kwa nidhamu ya mchezo, ni wakati gani wa kushambulia na wa kutulia, kumiki mpira au kupumzika, tukifanya hivi nadhani tutashinda mchezo wetu," alisema.

Kocha huyo amesema amekuwa akifuatilia mechi za wapinzani wao kila wanapocheza na leo usiku ataifuatilia Al Ahly ikicheza mechi ya Ligi Kuu Misri dhidi ya Smouha.

"Nimewafuatilia wapinzani wetu, wako vizuri tunatakiwa kuwa makini kwa sababu ya ubora wao, tulifanya makosa mechi iliyopita kwa kutokuwa na nidhamu ya mchezo na kupoteza.

Michezo
Jumanne Novemba 28, 2023
Nipashe



Newcastle kutupa ndoano Saudia UKURASA 22

TATIZO NINI?...



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, Salim Abdallah 'Try Again' (kulia), akiteta jambo na kiungo wa timu hiyo, Clatous Chama, baada ya juzi uongozi wa klabu hiyo kufanya kikao na wachezaji wote kutaka kujua shida ilipo kutokana na matokeo mabaya inayoyopata uwanjani. **PICHA: SIMBA**

## Gamondi ataka nidhamu kuivaa Al Ahly Jumamosi

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HUKU akiwataka wachezaji wake kucheza kufa kupona ili kupata matokeo katika mechi ijayo dhidi ya Al Ahly, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameeleza kilichosababisha kuangukia pua kwa mabao 3-0 nchini Algeria katika mechi yao ya kwanza hatua ya makundi dhidi ya CR Belouizdad.

Yanga itaikaribisha Al Ahly ya Misri Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, ambayo imetoka kushinda mabao 3-0 nyumbani dhidi ya Medeama ya Ghana.

Akizungumzia mechi dhidi ya Belouizdad na ijayo dhidi ya Al Ahly jijini Dar es Salaam jana, Gamondi alisema walipoteza mechi ya kwanza kutokana na makosa yao na mchezo ujao ni muhimu kupambana ili kupata matokeo chanya kwa sababu wakipoteza nyumbani dhidi ya Al Ahly watakuwa na kazi kubwa.

Aidha, amewataka wachezaji wake kupunguza makosa ambayo huwa yanafanyika kwenye mechi za Ligi Kuu na katika mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika uliochezwa nchini Algeria Ijumaa iliyopita dhidi ya CR Belouizdad.

Alisema kuna wakati wachezaji wake wanakuwa hawana nidhamu ya mchezo na kutaka kufanya vitu vingi visivyohitajika uwanjani, kitu ambacho katika mechi za Ligi Kuu huwezi kuadhibiwa kwa sababu ya baadhi ya viwango vya timu nyingi si bora, lakini vinakuja kuonekana na kuadhibiwa ukikutana na timu kubwa na bora.

"Nidhamu kwenye mch-

INAENDELEA UKURASA 23

# JWANENG, WYDAD KUAMUA HATIMA WAKUKATWA SIMBA

## Wachezaji, uongozi wakubaliana kuelekea dirisha dogo, huku kocha Benchikha akitua na...

**Na Saada Akida**

WACHEZAJI wa Simba wamepewa nafasi ya mwisho kuelekea mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana na ule wa Wydad Casablanca ya Morocco ili kuonesha kiwango kwa kupigania timu tofauti na hivyo, panga la dirisha dogo la usajili litawahusu, imefahamika.

**Hayo ni maadhimio yaliyofikiwa kati ya viongozi na wachezaji baada ya kikao kizito kilichokaliwa juzi usiku baada ya mazoezi katika kambi ya timu hiyo Mbweni, Dar es Salaam, kulingana na matokeo na viwango vibovu vilivyooneshwa katika mchezo dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast wiki iliiliyopita wakati wakitoka sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.**

Taarifa zilizoifikia Nipashe jana kutoka ndani ya klabu hiyo zimeeleza kuwa katika kikao hicho, kumejadiliwa mambo mbalimbali likiwamo matokeo mabaya ya mechi tatu zilizopita pamoja na mikakati kuelekea mechi ijayo dhidi Jwaneng Galaxy na ujio wa kocha ambao utaambatana na usajili wa dirisha dogo.

Mtoa habari huyo alisema uongozi umevunja ukimya na kuwaeleza wachezaji juu ya maadhimio yao kuwa mechi hizo mbili za kimataifa zilizopo mbele yao ni kipimo kwao kuonesha kiwango kizuri kuthibitisha nafasi yao ya kuendelea kusalia ndani ya kikosi hicho.

"Kikao cha kwanza kilifanyika Jumamosi baada ya dakika 90 na Asec Mimosas kukamilika, viongozi walichukizwa na kuwaeleza kuwa asiyetaka kujituma akamuona mtendaji mkuu apewe barua na haki zake, lakini hilo halikutokea.

"Lakini juzi viongozi waliamua kuibuka kambini na kuzungumza na wachezaji kuweka sawa na kila mmoja wao kujiwekea mikakati yao kuelekea mechi mbili za kimataifa tunazokwenda kucheza ugenini, ni nafasi kwa kila mchezaji kuonesha uwezo wake kuipigania timu kwa sababu ni mechi ambazo zitaamua hatima yake ya kusalia dirisha dogo litakapofunguliwa," alisema mtoa habari huyo.

Aliongeza kuwa hatua hiyo ni baada ya ujio wa Kocha Mkuu mpya, Abdelhak Benchikha anayetarajia kutua nchini muda wowote ili kuona timu yake na Alhamisi kuambatana nayo kuelekea Botswana kuivaa Jwaneng Galaxy.

"Tayari kocha amepewa makali yote kuhusu maboresho na atatumia michezo hiyo miwili ikiwamo dhidi ya Jwaneng Galaxy na Wydad Casablanca ya Morocco. Timu itaondoka na ndege ya kukodi hadi Botswana baada ya mechi kikosi kitaondoka kuelekea Morocco," alisema mtoa habari huyo.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again', kikao hicho kimemaliza kila kitu na kuweka sawa mambo yote, kazi iliyobaki ni wachezaji kwenda kutafuta matokeo chanya katika mechi mbili zilizopo mbele yao.

Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema wanafungua ukurasa mpya baada ya usiku wa kuamkia jana kuwapo kwa kikao maalum cha kujadili timu yao.

Alisema yote yaliyoonekana ni tatizo yamejadiliwa na kutafuta ufumbuzi kwa haraka ili kusonga mbele katika michezo iliyopo mbele yao.

"Kwa pamoja tumedhamiria kuzaliwa upya na kila mmoja kwenye eneo lake ameahidi kuongeza ubora, juhudu na ufanisi, sasa tutegemee mabadiliko chanya, tutarajie Simba mpya yenye ubora wa kutisha, yaani Simba yetu inarejea.

"Yaliyopita yamepita sasa tunafungua ukurasa mpya wa furaha, Wanasimba tupeni imani yenu hatutawaangusha uwezo wa kufanya vizuri tunayo na nafasi ya kusonga mbele katika michuano ya kimataifa ipo wazi," alisema Ahmed.

Wakati huo huo wachezaji wa Simba

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >